# Darubini ya Wiki

*Kwa mwenye bongo pevu* | Toleo Nambari 12 | Novemba 20, 2022 JARIDA LA JUMAPILI BILA MALIPO




# NITABOMOA UKUTA SOMALIA

**Ukuta wa kilomita 700 kuzuia Al-Shabaab? Hiyo ni mbinu ya kizamani na isiyofaa, anasema Waziri wa Ulinzi Aden Duale. Katika mahojiano na Darubini ya Wiki, Duale anaelezea mpango wake wa mfumo 'wa kisasa' wa usalama**

# *The Nation ePaper NOW Available on the PlayStore*

## anywhere, anytime.




Follow the link to subscribe

> *epaper.nation.africa.*

Scan to Download

Or download from Google playstore

ANDROID APP ON Google play

Nation

Nation

Nation Africa

For customer support Tel: 0790 111 111

Email: epaper@ke.nationmedia.com

NATION ePaper

kauli ya mhariri

## Yaliyomo


**5 ASALI SUMU YA SH17 BILIONI ZA KRA:** Rais Ruto auliza maswali magumu kuhusu kandarasi ghali ya mamlaka ya ushuru na kampuni ya Uswizi ambayo imekuwa ikiuzia mamlaka hiyo stampu za ushuru

**8 KDF:** KUKOMBOA AU KUFAIDI? Huku wanajeshi wa Kenya wakijiunga na juhudi za kulinda amani DRC, maswali yameibuka kuhusu nia halisi ya kutuma vikosi katika nchi yenye rasilimali nyingi inayokumbwa na mzozo

**16 SURA, AKILI NA SHERIA YA HAKIMILIKI:** Liz Lenjo aliona pengo na akaamua kulijaza, hatua iliyompeleka kuongoza Mahakama ya Hakimiliki Kenya.





**27 WAZIMU WA KOMBE TENA:** Katika siku 29 zijazo, ulimwengu mzima utaelekeza macho Qatar huku wanasoka bora - kutoka Ziyech, Neymar na Messi hadi Parley – wakikutana ana kwa ana kutafuta utukufu wa kimataifa


*- Zimetafsiriwa na Benson Matheka*

# Wanaokwepa kulipa ushuru ni lazima wafichuliwe, ni wezi wa ustawi wetu



**Washington Gikunju**

**Swali ni je, nani amekuwa akikusanya mabilioni haya yote yanayofaa kuwa yakifadhili ujenzi wa barabara nyingi za lami, maji ya mfereji nyumbani au dawa katika hospitali za umma? Jibu liko katika idara ya utekelezaji ya KRA kwa upande mmoja, na katika uadilifu wa mfumo na vifaa vinavyotumiwa kutengeneza stampu hizo za ushuru**

Stampu ya ushuru unayopata katika chupa yako ya maji, sharubati, pombe na mvinyo sio tu alama ya kuonyesha ushuru umelipwa lakini pia ni ishara ya hakikisho la ubora, kuonyesha kuwa bidhaa unayotumia sio haramu au pengine hatari kwa afya yako.

Baadhi ya takwimu zilizotolewa majuzi na Rais William Ruto, hata hivyo, zinazua wasiwasi na kupima imani yako katika stampu hiyo kama alama ya ubora.

Takwimu ambazo Rais Ruto alitoa majuzi katika siku ya walipaji ushuru zinaonyesha kuwa Uganda inauza stampu 9 bilioni za ushuru kila mwaka, Tanzania 7.2 bilioni ilhali Kenya inauza stampu 2.9 bilioni pekee.

Pato la Kenya, la karibu dola za Amerika 110.35 bilioni kulingana na makadirio ya Benki ya Dunia, ni zaidi ya jumla ya uchumi wa Tanzania (dola 67.78 bilioni) na Uganda (dola 40.43 bilioni).

Sekta ya utengenezaji bidhaa ya Kenya pia imestawi sana kuliko ya Tanzania na Uganda kumaanisha kuwa kuna bidhaa nyingi za kutozwa ushuru zinazotengenezewa Nairobi kuliko Dar es Salaam na Kampala.

Kwa hivyo, haiwezekani, kwa mujibu wa hesabu ya Rais Ruto, kwa Kenya kuuza karibu thuluthi moja ya stampu za ushuru ambazo Mamlaka ya Ushuru ya Uganda inauza kwa mwaka.

Rais anakadiria kuwa a KRA inafaa kuwa ikiuza kati ya stampu 10 bilioni na 12 bilioni kwa mwaka.

Hii ni muhimu sana kwa sababu inamaanisha ongezeko kubwa, la mabilioni, katika kiasi cha ushuru unaokusanywa na KRA.

Sasa swali ni, ni nani amekuwa akikusanya mabilioni haya yote ambayo yanafaa kuwa yakifadhili ujenzi wa kilomita nyingi za barabara za lami, maji ya mfereji katika nyumba au dawa katika hospitali za umma?

Jibu liko katika idara ya utekelezaji ya KRA kwa upande mmoja, na pia katika uwezo na uadilifu wa mfumo na vifaa vinavyotumiwa kutengeneza stampu hizo za ushuru.

Wanaokwepa kulipa ushuru ni wajanja kiasi cha kufahamu kuwa kujaribu kupenyeza katika soko bidhaa zinazotozwa ushuru bila stampu hizo ni njia rahisi ya kunaswa na kuonja nguvu za ukatili wa KRA, ikiandamana na polisi wenye silaha na kamera za televisheni.

Wanachofanya wakwepaji hao ni kutafuta nakala halisi ya stampu za ushuru na kuzibandika katika bidhaa zao, wakijua vyema kuwa hazina thamani kwa hazina. Matapeli hao huwa makini sana, hivi kwamba, kwa kutazama tu kwa macho, huwezi kutambua tofauti kati ya stampu iliyowekwa katika chupa ya vodka inayotengenezwa na kampuni ya East African Breweries na nyingine iliyotengenezewa katika eneo linalofahamika kama Kariobangi Light Industries.

Kama inavyofichua habari kuu ya kibiashara katika toleo hili la wiki hii, kandarasi ya kuuza stampu za ushuru imekuwa ikitengewa kampuni moja tu ya Ulaya kwa zaidi ya miaka kumi iliyopita.

Kandarasi hiyo kubwa iliongezwa muda kwa siri katika siku za mwisho za serikali ya Rais Uhuru Kenyatta, kupatia kampuni hiyo udhibiti mkubwa zaidi wa kutengeneza stampu hizo.

Zaidi ya uchunguzi unaoendelea kuhusu kandarasi hii inayoonekana kuwa mzigo mzito, uchunguzi pia unafaa kufanywa kujua ni kwa nini ni rahisi sana kuwa na stampu hizi feki.

Uchunguzi huo unafaa kuhusisha kubaini uwezekano wa njama kati ya wafanyakazi tapeli na wanaokwepa kulipa ushuru.

Kilicho muhimu zaidi, hatimaye, ni kuwa KRA inafaa kupata mgao wake halali wa ushuru, kusaidia kuleta maendeleo kote nchini na sio kunufaisha wahalifu wachache tu.

***wgikunju@ke.nationmedia.com***

*- Imetafsiriwa na Benson Matheka*


Darubini Ya Wiki

Lilianzishwa na marehemu Hillary Boniface Ngweno

**Stephen Gitagama** Afisa Mkuu Mtendaji
**Joe Ageyo** Mkurugenzi wa Uhariri

**Washington Gikunju** Mhariri Msimamizi, Wikendi
**Mike Owuor** Mhariri Jumapili
**Allan Buluku** Mhariri wa Weekly Review
**Njoki Ndung'u** Mhariri wa Uchapishaji

**Andrew Anini** Msanifu Kurasa Mkuu
**Joan Pereruan** Mhariri wa Picha
**Humphrey Osoro, Alice Othieno** Wasanifu Kurasa

darubini

■ Makamishna walikana matokeo ya kura

# 'Opaque 4' kuhojiwa na Wabunge

Makamishna wanne wa IEBC ambao walijitenga na matokeo ya uchaguzi wa urais wa Agosti 9 yaliyotangazwa na mwenyekiti Wafula Chebukati wanatarajiwa kufika mbele ya kamati ya Bunge la Kitaifa Kuhusu Masuala ya Haki na Kisheria kuhusu kesi zaidi ya nne za kutaka watimuliwe ofisini.

Wanne hao ni naibu mwenyekiti Juliana Cherera na makamishna Francis Wanderi, Irene Masit na Justus Nyang'aya.

Kamati inakagua kesi hizo kwa lengo la kuandaa ripoti itakayotoa mwelekeo kwa Bunge kuhusu iwapo malalamishi hayo yanatimiza viwango vinavyohitajika ili kuondoa mmoja au makamishna wote waliotajwa.

Wanne hao watajua hatima yao wiki ijayo ambayo kamati hiyo inatarajiwa kuwasilisha ripoti yake kuhusu iwapo Bunge litamtaka Rais William Ruto kuunda jopokazi maalumu la kubaini iwapo wanapaswa kutimuliwa ofisini kuambatana na Kifungu 251 cha Katiba.



Kutoka kushoto: Makamishna wa IEBC Francis Wanderi, Juliana Cherera (naibu mwenyekiti), Justus Nyang'aya and Irene Masit katika Hoteli Serena, Nairobi, mnamo Agosti 16.

■ Namba 5 Duniani Dubai kwa World Tour




Jon Rahm wa Uhispania ametaja mfumo mpya wa viwango vya dunia katika mchezo wa gofu kuwa "wa kuchekesha". PICHA | AFP

# Rahm asema viwango 'vinachekesha'

Jon Rahm ametaja mfumo mpya wa wa viwango vya wachezaji wa gofu duniani kuwa 'wa kuchekesha' baada ya kumaliza msimu wa mashindano DP World Tour unaokamilika wiki hii kwa nusu ya pointi zilizopatikana katika mashindano ya PGA Tour nchini Amerika.

Rahm, nambari tano duniani, ni miongoni mwa wachezaji maarufu walio Dubai kushindania dola 10 milioni za Amerika (karibu Sh1.2 bilioni) katika mashindano ya Ubingwa wa DP World Tour. Kikosi hicho thabiti cha wachezaji 50 nyota wanaoshiriki mashindano ya Dubai mwaka huu, kinaongozwa na nambari moja Rory McIlroy na kujivunia wachezaji wanane kutoka kwa 30 bora duniani.

Kwa kulinganisha, kikosi cha PGA Tour RSM Classic katika jimbo la Georgia kina wachezaji wanne tu wa gofu kutoka kwa 30 bora, huku nambari 12 Tony Finau akiwa mshindani wake bora zaidi. Wachezaji 156 wanaojiandaa kumenyana katika Kisiwa cha Sea wanajumuisha nambari 915 Chris Stroud na mchezaji mkongwe Davis Love III, ambaye ni nambari 2,856. "Nitasema wazi, nafikiri kwa sasa OWGR inachekesha," akasema Rahm kabla ya shindano la Mashariki ya Kati. "Naelewa wanachojaribu kufanya kutokana na hali ya uwanja. Lakini wachezaji 30 bora duniani wa mwaka huu hawastahili kuadhibiwa kwa sababu uwanja ni mdogo," akasema Rahm.

■ Jaji alisitisha upigaji msasa Jumanne

# Korti kuamua hatma ya Makatibu



Macho yote yatakuwa kwa Mahakama ya Uajiri na Mahusiano Kazini jijini Nairobi Jumatatu, ikitarajiwa kuamua kuhusu upigaji msasa wa watu 51 walioteuliwa na Bunge la Kitaifa kuwa Makatibu wa Wizara.

Kesi hiyo iliyowasilishwa na Chama cha Wanasheria Kenya (LSK), itasikizwa Novemba 21, mbele ya Jaji Nzioki wa Makau. Mahakama Kuu Jumanne iliyopita ilisitisha shughuli ya kupiga msasa makatibu wa wizara walioteuliwa baada ya LSK kulalamika kuhusu orodha hiyo, ikisema haizingatii usawa wa kiameneo na kikabila, sheria kuhusu ujumuishaji wa jinsia, walemavu na vijana.

■ Bosi wa Fifa kusimama bila mpinzani

# Infantino atagombea muhula wa tatu



Rais wa Fifa Gianni Infantino atagombea bila mpinzani kwa muhula wa tatu kuwa mkuu wa shirika la kandanda duniani mwaka ujao, Fifa imethibitisha. Taarifa fupi kutoka Fifa ilisema Infantino atakuwa mgombeaji pekee chaguzi zikifanywa katika Kongamano la 73 la Fifa jijini Kigali, Rwanda mnamo Machi 16. "Hakuna mgombeaji mwingine," ikasema taarifa.

Muhula wa tatu wa Infantino unafuata mkondo wa marais wa Fifa waliotangulia - Joao Havelange kutoka 1974 hadi 1998 na Sepp Blatter kutoka 1998 hadi 2015. Infantino alichaguliwa 2016 akiahidi "kurudisha sifa ya Fifa" baada ya shirika hilo kukumbwa na kashfa katika miaka ya mwisho ya uongozi wa Blatter.

*- Zimetafsiriwa na Mary Wangari*

Nation Media Group "Digital Copy"

kurunzi ya kenya

■ HUENDA RAIS AKAAGIZA UCHUNGUZI KUHUSU STAMPU FEKI

## Ruto auliza maswali magumu kuhusu kandarasi ghali ya mamlaka ya ushuru na kampuni ya Uswizi ambayo imekuwa ikiuzia mamlaka hiyo stampu za ushuru




# ASALI SUMU YA SH17BN ZA KRA

● Na JAINDI KISERO

Jina Sicpa Solutions huenda lisiwe maarufu Kenya. Lakini huenda kwa wakati mmoja watumiaji wengi nchini walinunua bidhaa zilizo na bidhaa zinazotengenezwa na kampuni hiyo: Stampu za ushuru ambazo hubandikwa katika kila chupa ya sharubati, maji, pombe, bidhaa za urembo, na bidhaa za tumbaku.

Stampu hizo zinazouzwa na Mamlaka ya Ushuru Kenya (KRA), zinaruhusu mamlaka hiyo ya ushuru kuthibitisha uhalali wa bidhaa na kudhibitishia KRA kuwa ushuru uliohitajika umelipwa. Rais William Ruto hivi majuzi amekuwa akilalamika kuhusu anachotaja kuwa idadi ya chini ya stampu za ushuru zinazouzwa Kenya.

Akihutubu mwezi jana wakati wa maadhimisho ya siku ya mlipa ushuru mwaka huu, Rais Ruto alishangaa ni kwa nini Kenya - ikiwa na uchumi mkubwa kuliko nchi jirani za Uganda na Tanzania, inauza stampu chache kuliko mataifa mengine wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Takwimu ambazo Rais Ruto alifichua katika siku ya mlipa ushuru ni kama ifuatavyo. Kulingana naye, Uganda huuza stampu za ushuru za thamani ya Ksh 9 bilioni kila mwaka, Tanzania KSh7.2 bilioni na Kenya kiasi kidogo cha KSh2.9 bilioni.

Katika makadirio ya Rais mwenyewe, Kenya inafaa kuwa ikiuza stampu za kati ya Sh10 bilioni na Sh12 bilioni kila mwaka, kwa kuzingatia ukubwa wa sekta yake ya viwanda.

Kabla ya wiki kuisha, Rais aliibua suala hilo tena akihutubia mkutano wa Chama cha Watengenezaji Bidhaa Kenya (KAM) katika hoteli moja ya Nairobi. Katika hafla hiyo, alisema kuwa Kenya inauza stampu nyingi feki kuliko halali.

Kama mbavyo ingetabiriwa, jinsi Rais amekuwa akizungumzia suala hilo, imeibua tena sio tu suala la idadi ya stampu za ushuru ambazo KRA huuza, lakini pia swali kuhusu thamani ya pesa za kandarasi ambayo kampuni hiyo kubwa ya Uswizi, imekuwa ikitoa

Endelea Uk 6

Nation Media Group "Digital Copy"

kurunzi ya kenya

# Mkataba wa kushangaza kati ya KRA na Sicpa

Kutoka Uk 5

teknolojia na stampu kwa KRA tangu Aprili, 2013.

Kwa mtazamo wowote ule, kile ambacho Rais Ruto aligusia ni suala kubwa sana kwa sababu ya ukubwa wa kandarasi hiyo, suala tata kuhusu thamani ya pesa ambalo limezonga kandarasi ya Sicpa tangu ilipotiwa saini karibu miaka kumi iliyopita - na kubwa zaidi ni ukweli kuwa kandarasi hii inaaminika kuhusisha watu maarufu katika utawala wa Rais Mstaafu Uhuru Kenyatta.

Imekuwa ikishukiwa kuwa matamshi ya Rais Ruto yanaonyesha uchunguzi utafanywa kuhusu suala la stampu za ushuru. Je, usaidizi wa kisiasa ambao kampuni hiyo ya Uswizi ilifurahia chini ya utawala wa Rais Kenyatta unafifia? Hili ni swali lingine ambalo wachanganuzi wengi wanauliza.

Suala hili limeibua hisia za umma na umakinifu kwa sababu kandarasi zinazohusu uchapishaji wa stampu za ushuru - kama ilivyo kwa kandarasi za kuchapisha noti za pesa - huwa zinakumbwa na utata na madai ya ufisadi.


Ukweli ni kuwa kandarasi ya Sicpa yenyewe inayojumuisha mfumo wa ufuatiliaji unaofahamika kama EGMS, imekuwa tangu mwanzo ikikumbwa na utata ambao umedumu kwa miaka mingi na kuhusisha karibu asasi zote kubwa za serikali ikiwemo Wizara ya Fedha, Afisi ya Rais, Mahakama ya Rufaa Kuhusu Ununuzi wa Bidhaa za Umma na Bunge.

Katika hali ya sasa, inaonekana kilichovutia umakinifu wa serikali mpya ya Rais Ruto ni maamuzi ya kutiliwa shaka yaliyofanywa kuelekea mwisho wa serikali iliyoondoka kwa kuwa kandarasi hiyo ya mabilioni ya pesa ilikuwa imekaribia kuisha na hata waliokuwa na usemi katika serikali hiyo na Sicpa walianza kukubali uwezekano wa utawala kubadilika.

Stakabadhi zilizoonekana na Darubini ya Wiki zinaonyesha kuwa mnamo Mei mwaka jana, kampuni hiyo ya kimataifa ya Uswizi ilifaulu kujadili mkataba mpya wa pesa nyingi uliofungia nje washindani na kuiwezesha kuendelea kupata kandarasi za kuchapisha stampu za ushuru kutoka KRA bila kujali serikali iliyo mamlakani.

Stakabadhi zinaonyesha kuwa KRA ilitia saini mkataba wa ziada kwa uliokuwepo wa miaka saba wa Sicpa - lakini ukweli ni kuwa ulikuwa mpango wa kufunga mamlaka hiyo ya ukusanyaji ushuru kuondoa ushindani kwa kampuni hiyo iliyokuwa imetoa huduma hizo kwa muda mrefu.

Kwenye kandarasi mpya iliyotiwa saini mnamo Mei 4, 2021, KRA ina mambo matatu muhimu. Kwanza, Sicpa iliahidi kukabidhi KRA mfumo wa EGMS na vifaa bila malipo. Hatua hiyo inaweza kuonekana kuwa ukarimu wa kampuni hiyo. Lakini kwa upande mwingine ni kuwa teknolojia hii na vifaa hivyo vya miaka 10 vimepitwa na wakati.



Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Ushuru Kenya Githii Mburu. Katika mkataba mpya uliotiwa saini mnamo Mei 4, 2021, Sicpa ilikubali kupatia KRA mfumo wa ufuatiliaji wa EGMS na vifaa vingine bila malipo.KRA na Sicpa zilikubaliana 'kutoa mfumo wa EGMS kwa mashirika mengine ya serikali".

Lakini hatari zaidi inapatikana katika sehemu ya pili ya mkataba huo. Katika makubaliano hayo, KRA ilitia saini kandarasi ya utengenezaji inayojumuisha uuzaji wa stampu, wino wa kuweka alama, vipuri vya vifaa vilivyowekwa katika kampuni za kutengeneza bidhaa na mifumo ya kusimamia data.

Sicpa imepewa kandarasi ya kuboresha mifumo na huduma zingine ambazo KRA inaweza kuhitaji kuwezesha mfumo huo kufanya kazi ipaswavyo.

Katika kandarasi ya zamani, bei ya stampu ilikuwa isiyobadilika. Kandarasi mpya ilianzisha mpango mwingine ambao unatoa bei ya chini bila kuweka bei ya juu, huku ukiacha bei ya stampu kutegemea bei za kimataifa.

Ni hali ambayo mwanakandarasi wa muda mrefu anaruhusiwa kutumia KRA kunufaika na kuzuia mamlaka hiyo kupata kampuni zingine za kutoa huduma hizo.

Lakini pengine kile kinachoeleza vyema kiwango cha juu cha ukarimu wa kisiasa ambacho kampuni hiyo ya Uswizi ilikuwa ikifurahia chini ya serikali ya Rais Uhuru Kenyatta ni njama na mipango ya kamati iliyokuwa ikishirikishwa kutoka Afisi ya Rais na kundi lenye jina refu la Kundi la Kiufundi la Mashirika Tofauti Kuhusu Mfumo Uliopendekezwa wa Kuweka Alama Bidhaa na Kuzithibitisha.

Kile ambacho kamati hii ilikuwa ikipendekeza kuanzisha ni kitu kinachoitwa "Alama Jumuishi ya Serikali ya Kenya". Kwamba, badala ya hali ya sasa ambapo mashirika kadhaa, ikiwemo KRA, Kebs, KEPHIS, na Mamlaka ya Kupambana na Bidhaa Feki yanayohusika na uthibitishaji wa bidhaa na utoaji wa stampu za ushuru, Kenya ilichohitaji ni mfumo mpya ambapo uidhinishaji wa bidhaa na stampu za ushuru zinapaswa kuwekwa pamoja na kuendeshwa katika jukwaa moja chini ya mfumo wa EGMS wa KRA unaosimamiwa na Sicpa.

Ili kufanikisha kisheria pendekezo hilo, kamati ilikuwa imetayarisha Mswada wa Alama Jumuishi ya Serikali ya Kenya, 2022, ambao ulinuiwa kutolewe na KRA.

Ikiwa hii ilikuwa njama ya kupatia Sicpa ukiritimba wa kuchapisha stampu za mashirika yote ya serikali Kenya ni swali lililo na jibu wazi, mpango huo ulikuwa wa kunufaisha Sicpa pakubwa.

Kile kinachofanya wadadisi kuamini kuwa mpango wa kuunda alama moja ya serikali ulikuwa dhihirisho lingine la uungwaji wa kisiasa ambao Sicpa ilifurahia chini ya utawala wa Rais Uhuru Kenyatta ni ukweli kuwa hata kabla ya sheria ya kuunda alama ya pamoja ya serikali ya Kenya kupitishwa, maamuzi yalikuwa yakifanywa haraka kuweka mashirika mengine chini ya mfumo wa EGMS unaosimamiwa na Sicpa.

Kwa mfano, Sicpa na KRA ziliruhusiwa kufanikisha mpango huo ambao mashirika mengine yalitakiwa kupatia EGMS kandarasi za kuchapisha stampu.

Katika mpango huo mpya, KRA na Sicpa zimeahidi 'kuhakikisha mfumo wa EGMS unapatikana kutumiwa na mashirika mengine ya serikali'. Na katika stakabadhi za kandarasi, kuna vipengee vinavyoeleza fomula ya kutathmini bei ya mashirika mengine ya serikali ambayo yatakuwa yamejiunga na jukwaa la EGMS katika KRA. Pia, kipengee kingine kinasema kuwa KRA na Sicpa zitatoa huduma za kusaidia uchunguzi na mashtaka kwa maafisa wa Kenya na mashirika ya utekelezaji.

Ukweli kwamba Sicpa na KRA zilitia saini mpango ambapo mfumo wa EGMS unaosimamiwa na Sicpa ungekuwa wa pekee kutoa stampu, zikiwemo bei - kwa mashirika mengine ni moja ya sehemu za kuvutia kuhusu sakata hii.

Darubini ya Wiki pia imeona mawasiliano yanayoonyesha kwamba hata kabla ya mswada wa alama ya serikali ya Kenya kupitishwa, KRA ilikuwa ikiandikia Wizara ya Fedha ikitaka idhini ya kuruhusiwa kununua stampu zake za usalama za uagizaji bidhaa kupitia mfumo wa EGMS wa Sicpa. Meneja wa Sicpa humu nchini, Lilian Atogo, alikataa kuzungumzia masuala yaliyongaziwa katika habari hii, akisema wateja wa Sicpa - KRA na serikali ndio wanafaa kujibu maswali kuhusu mikataba hiyo.

*- Imetafsiriwa na Benson Matheka*

Nation Media Group "Digital Copy"

kurunzi ya kenya

RAHISISHA USAJILI WA BIASHARA

# UKWELI MCHUNGU WA PESA ZA HASLA

## Wataalamu wa kibiashara wanasema fedha hizo zinafaa kutolewa kupitia vyama vya ushirika na vya kibiashara, ambako mshikamano na uwajibikaji katika kulipa mikopo ni wa kiwango cha juu

• NA MACHARIA GAITHO

Huku serikali ikianza mipango yake ya kubuni Hazina ya Hasla na mikakati mingine ili kusaidia biashara ndogo, hali ya kutamausha imekumba watu waliotarajiwa kufaidika.

Kulingana na Afisa Mkuu Mtendaji wa Muungano wa Biashara Ndogo na Kadri, Bw Sammy Karanja, Waziri wa Biashara na Uwekezaji Moses Kuria alikuwa akijipiga kifua kwa kauli yake ya kukanganya kuhusu nguo za mitumba.

Mapema mwezi huu, Kuria alirudi nchini kutoka Afrika Kusini, na kusema kuwa uagizaji wa nguo hizo umepigwa marufuku ili kuimarisha utengenezaji nguo na vitambaa humu nchini.

Baada ya ripoti na hisia kuibuka kuwa Waziri alilenga kupiga marufuku mitumba, hasa katika mitandao ya kijamii, Kuria alibadili kauli yake. Akidai alinukuliwa vibaya, alifafanua kuwa anacholenga ni kuhakikisha biashara ya mitumba ni ghali kuendesha kupitia utozaji ushuru na taratibu nyingi za kuihalalisha.

Hivyo, nguo hizo hazitakuwa njia pekee ambayo Wakenya wanaweza kupata mavazi yao, bali watakuwa wakinunua nguo zilizotengenezwa nchini, ili kukuza viwanda nchini.

Lakini kulingana na Karanja, Kuria anafanya mambo kwa utaratibu usiofaa, kwani watengenezaji nguo na vitambaa hawana uwezo wa kukidhi mahitaji ya nguo za viwango vya juu na bei rahisi nchini. Jambo linalofaa kupewa kipaumbele ni kuongeza uzalishaji hapa nchini na baadaye kuwaruhusu wateja kufanya maamuzi kutokana na nguo zilizo sokoni, iwe zimetengenezwa nchini au zimeagizwa kutoka nje.

Anasema kuwa biashara ya mitumba husaidia watu milioni nne kwenye utaratibu mzima wa uagizaji, usafirishaji, usambazaji na uuzaji, hivyo haipaswi kufungwa bila kuwepo kwa biashara mbadala.

Kinaya ni kuwa, msimamo wa serikali kuhusu mitumba, iwe ni kuzipiga marufuku au kufanya nguo hizo kuwa ghali kama njia ya kulinda viwanda nchini, unawiana na msimamo wa kiongozi wa upinzani Raila Odinga wakati wa kampeni za urais.

Mrengo wa Kenya Kwanza, wa Rais William Ruto, ulimkosoa sana Odinga alipopendekeza vikwazo dhidi ya uagizaji mitumba ili kutoa nafasi ya kufua viwanda vya nguo nchini na kubuni ajira.

Odinga alilaumiwa kwa kupendekeza njama ya kumaliza biashara za mahasla, ikizingatiwa kuwa bidhaa wanazouza zinazotumika kwa wingi na watu wa mapato ya chini.

Msimamo kuhusu mitumba unaashiria uhalisia unaokumba ahadi za mikopo ya hasla bila riba, masharti yasiyo magumu ya ushuru, uondoaji vikwazo katika uagizaji bidhaa kuukuu miongoni mwa ahadi nyingine za kampeni ya Ruto.

Uhalisia mchungu ulianza kudhihirika mara tu baada ya utawala mpya kuchukua uongozi. Bila shaka mahasla waliotarajia kupewa pesa kuinua biashara zao ndogo walikumbwa na mshangao baada ya kanuni zitakazotumiwa kudhibiti Hazina ya Hasla kuchapishwa. Hazina hiyo itaendeshwa kwa kuzingatia Kanuni za Usimamizi wa Fedha za Umma (Hazina ya Ushirikishi wa Fedha).



Hiyo ina maana kuwa hakutakuwa na pesa za bure, lakini mikopo itakayotozwa riba ya asilimia nane. Hicho ni kiwango kizuri ikilinganishwa na viwango vinavyotozwa na benki, kwani vingi ni zaidi ya asilimia kumi.

Kutakuwa pia na masharti magumu ya kupata pesa hizo, kiwango cha juu zaidi kutolewa kikiwa Sh50,000 kwa kila ombi, kiwango ambacho kimekosolewa na wengi na kufanya wanablogu wa Kenya Kwanza kukitetea.

Kilicho wazi ni kuwa Hazina ya Hasla itatolewa kwa masharti magumu yanayolenga kuhakikisha Pesa hizo zimetumiwa vizuri na kwa uwajibikaji mkubwa, ili kuepuka uwezekano wa wakopaji kushindwa kulipa. Mfumo wa usimamizi wake na masharti yaliyowekwa yanaonekana kuepuka matatizo yaliyokabili mipango kama hiyo hapo awali kama vile Hazina za Wanawake na Vijana, iliyogeuka pesa za kufaidi wanasiasa kwani zilitolewa bila kutarajiwa kulipwa. Pia, ilisimamiwa kwa ufisadi na mpangilio usiofaa, hali iliyosababisha hasara kubwa kwani maafisa wakuu walipora pesa nyingi zilizokuwepo.

Kuna suala la ushuru pia. Kinyume na dhana iliyokuwepo kuwa wafanyabiashara wadogo wangepata afueni, serikali haitawahurumia kwani inafanya juu chini kuongezea sehemu za kupata ushuru ili kufikia bajeti yake.

Rais Mstaafu Uhuru Kenyatta alipoteza ngome yake ya Mlima Kenya kutokana na propaganda eti alikuwa akiua biashara ndogo kufuatia msako wa serikali dhidi ya ulanguzi, kutolipa ushuru na uagizaji wa bidhaa ghushi na ambazo hazijafikisha viwango vinavyofaa vya ubora.

Ingawa serikali ya Kenya Kwanza

Endelea Uk 9

Nation Media Group "Digital Copy"

kurunzi ya kenya

VITA NCHINI CONGO

# KDF: KUKOMBOA AU KUFAIDI?

**Huku Jeshi la Ulinzi Kenya (KDF) likijiunga na juhudi za kuleta amani DRC, maswali mapya yanaibuka kuhusu nia hasa ya nchi zinazotuma wanajeshi katika nchi hii inayokumbwa na vita na yenye utajiri wa mali asili**

Na KWENDO OPANGA

Akitembea mjini Goma, mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), wiki jana, rais mstaafu Uhuru Kenya, ambaye sasa ni balozi wa amani wa DRC kwa niaba ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), alizingirwa na watu waliopoteza makao wakitaka kumsimulia masaibu yao mikononi mwa M23, wahusika wakuu katika vita kati ya DRC na waasi.

Mapigano DRC na kuingilia kati kwa mataifa jirani sio jambo geni. Mnamo 1998 Zimbabwe, Angola na Namibia ziliingilia kati kijeshi kuzuia kung'olewa mamlakani kwa Rais Joseph Kabila na muda mfupi baadaye mwanawe, Laurent, na waasi walioungwa mkono na Rwanda na Uganda.

Wakati huu, wanajeshi kutoka Kenya, Uganda, Burundi na Sudan Kusini wameingilia mapigano mashariki mwa DRC eneo lenye utajiri mkubwa wa madini, kukomesha mapigano kati ya waasi wenye silaha na wanajeshi wa serikali ya Rais Felix Tshisekedi. Wanalenga kurudisha amani na kuwapokonya silaha waasi hao.

Mnamo 1998, vikosi vya kuleta amani vilifanya hivyo chini ya usimamizi wa nchi wanachama wa Jumuiya ya Ustawi wa Mataifa ya Kusini mwa Afrika (SADC) na wakati huu ni zamu ya EAC.

EAC haikuwepo 1998, kwani ilisambaratika 1977. Na Machi mwaka huu, DRC ilijiunga na jumuiya hiyo (EAC) na kufikisha idadi ya wanachama wake kuwa saba na kupatia jumuiya hiyo sababu ya kuingilia kati mizozo yake ya ndani.

DRC ambayo ndiyo nchi ya pili kwa ukubwa Afrika baada ya Algeria, inapakana na nchi tisa, ambazo ni; Angola, Burundi, Rwanda, Uganda, Jamhuri ya Congo, Jamhuri ya Afrika ya Kati, Sudan Kusini, Tanzania na Zambia. Kenya inatekeleza wajibu mkubwa katika juhudi za kurudisha amani DRC, katika mchakato ulioanzishwa Machi mwaka huu na Kenyatta na ambao umekumbatiwa na mrithi wake, William Ruto, na marais wa nchi wanachama wa EAC.



Meja-Jenerali Jeff Nyagah (kulia), kamanda wa kikosi cha Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), akisalimia wanajeshi wa Kenya baada ya kufika katika makao makuu ya EAC kwa mkutano na wanahabari mjini Goma, mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo mnamo Novemba 16. PICHA I AFP

Akituma kikosi cha kwanza cha wanajeshi 900 wa KDF kwenda DRC, Rais Ruto alisema wazi kuwa, "kama majirani wenye mahusiano mbalimbali, hatima ya DRC imeingiliana na yetu. Sote tutafaidika na uthabiti wa DRC na usalama wake ni wajibu ambao tumejitolea kutimiza."

Jumuiya ya EAC inaonekana imeiga SADC kwa kuingilia mapigano DRC. Kulingana na Shirika la Kusuluhisha Mizozo Afrika, (ACCORD), "kushiriki kwa mashirika ya Afrika katika juhudi za kuleta amani DRC zimejikita katika utambuzi kuwa huenda mapigano hayo yakasahauliwa na kuendelea kwake kutazaa utamaduni wa ghasia."

ACCORD iliongeza kuwa hatua ya SADC kuingilia mzozo DRC ilionyesha haja ya Umoja wa Afrika na mashirika ya kanda kuwa wa kwanza kuingilia mapigano katika ukanda huo kupitia juhudi za kidiplomasia, mazungumzo, operesheni za amani, kulinda amani, kurudisha utulivu na ujenzi upya wa nchi baada ya mapigano.

Kenya inaonekana kuelewa wajibu huu. Kabla ya Rais Ruto kutuma KDF nchini DRC, Waziri wake wa Kigeni na Masuala ya Ughaibuni, Alfred Mutua aliambia "Darubini ya Wiki" Kenya imejitolea kuendeleza amani nchini Ethiopia, Somalia, Sudan Kusini na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo "kwa sababu ni kupitia amani na uthabiti wa kisiasa katika eneo hili ambapo ustawi wa kiuchumi utapatikana" na kuwa "ufanisi wa DRC, nchi yenye mbao, uwezo wa kuzalisha umeme kutokana na maji na ardhi yenye rotuba na madini, utakuwa ufanisi kwa eneo hili."

Akikariri kauli hizo, Bw Aden Duale, Waziri wa Ulinzi, aliambia Darubini ya Wiki kwenye mahojiano tofauti katika toleo hili kuwa Kenya inafurahia kushiriki juhudi za amani DRC kwa sababu kadhaa, "ikiwemo kuwa tunawekeza katika amani katika eneo hili na kutokana na hilo, tutafaidi."

Akitetea kutumwa kwa KDF nchini DRC, mbele ya wabunge, Bw Nelson Koech, mwenyekiti wa Kamati ya Bunge Kuhusu Ul-

Nation Media Group "Digital Copy"




Wanajeshi wa Congo wakilinda uwanja wa ndege mjini Goma, DRC, mnamo Novemba 15.PICHA I AFP

inzi na Masuala ya Kigeni, aliambia gazeti la "The East African", kuwa, kupitia mchakato huo, Kenya itaendeleza maslahi yake makuu, zikiwemo biashara kama vile benki zinazohudumu DRC, wafanyabiashara wengi Wakenya nchini humo, biashara kati ya Kenya na DRC na matumizi ya bandari ya Mombasa na DRC, miongoni mwa mengine.

Lakini suala kuu ni kuwa Kenya na KDF wanaingia vitani. Vita vinagharama za kifedha, na za kibinadamu.

Pili, vita vinapoanza hushika kasi na huenda vikaelekeza wapiganaji katika mkondo ambao hawakutarajia. Ni baada ya miaka minne ambapo SADC ilianza kupunguza vikosi vyake DRC.

Vikosi vya kulinda amani vya Umoja wa Mataifa (UN) vimekuwa DRC kwa miaka 22, lakini havijaleta amani katika nchi hiyo. Wakati huu wanachukiwa na wakazi ambao wanataka waondolewe.

Kenya inakadiria kuwa itagharimu Sh6 bilioni kwa wanajeshi wake kuwa nchini DRC kwa miezi sita. Hiyo ni gharama kubwa kwa uchumi ambao umeathiriwa na Covid-19, umezongwa na madeni na unakumbwa na kupanda kwa bei ya bidhaa za kimsingi. Lakini kulingana na Duale, katika taarifa yake kwa bunge kuhusu maana ya kutuma KDF nchini DRC, huenda gharama ya kutochukua hatua ikawa kubwa zaid kuliko hiyo, kauli iliyokubaliwa na Bunge.

Tatu, kuna hatari katika hatua hiyo. UN ilishutumu vikosi vya kijeshi vilivyotumwa DRC katika miaka ya '90 kwa kupora rasilimali za madini nchini humo.

Ripoti tofauti ilisema wanajeshi wa Zimbabwe walibinafisisha na kuendesha shughuli za uchimbaji madini nchini DRC.

Jason Stearns, Profesa katika Chuo Kikuu cha Fraser, Canada, mwanzilishi wa Congo Research Group na mwandishi kuhusu DRC, alishutumu Rwanda na Uganda kwa kupora dhahabu na madini mengine nchini DRC.

Nne, DRC na Rwanda zinalaumiana kuhusu mapigano mashariki mwa DRC, huku serikali ya Rais Tshisekedi ikidai Rwanda inatoa msaada wa kivita kwa wapiganaji wa M23. Nayo Rwanda inailaumu DRC kwa kutoa makao kwa wanamgambo wa Democratic Front for the Liberation of Rwanda.

Mwaka jana Uganda ilipeleka wanajeshi mashariki mwa DRC kupigana na wafuasi wa kundi la Allied Democratic Forces (ADF), inaowalaumu kwa kushambulia kwa mabomu maeneo ya mji wa Kampala.

Tano, matokeo yake ni kuwa wahusika wawili katika machafuko DRC, Uganda na Rwanda, pia ni washirika katika mchakato wa amani unaoongozwa na Kenya. Nchi hizo zimetuma wanajeshi DRC, ingawa Rwanda imejikita katika huduma za uchukuzi pekee na wanajeshi wake hawaruhusiwi DRC. Ni hali tata lakini inayoruhusu wahusika kuendelea kufyonza rasilimali za DRC.

Mwisho, mlipuko wa vita juzi mashariki mwa DRC unachangiwa na sababu kuwa serikali ya nchi hiyo ni dhaifu na wanajeshi wake hawawezi kuwakabili waasi hao. Kulingana na Stearns, Tshisekedi alipozuru mashariki mwa DRC mara ya kwanza, alitaja wanajeshi wake kuwa "mafia" na kulalamika kuwa nchi anayoongoza imekufa.

M23 walianza vita mwaka jana kwa sababu, wanasema, DRC ilikaidi makubaliano nao baada ya kukomeshwa kwa vita mnamo 2013. Mapigano hayo yanalenga kulazimisha DRC kutimiza ahadi yake kulingana na makubaliano hayo ya 2013, wakati ambapo, inakumbukwa, M23 walishindwa.

Ni sawa kwa hivyo, kwa hatua za kijesho kuambatanishwa na mbinu za kidiplomasia. Hii ndiyo sababu Kenyatta alizuru Kinshasa na Goma wiki jana, lakini usimamizi wa amani na ujenzi upya baada ya mapigano sharti yawe kwenye ajenda ya EAC.

Na pendekezo hili la Koech pia: "Baada ya kutuma kikosi cha kwanza cha wanajeshi, tunaweza kuvuta ufadhili na presha kwa Hazina ya Kitaifa itapungua. Vikosi vya usalama ni ghali. Sharti tuhakikishe wanajeshi wetu wana silaha bora za kumaliza mapigano yaliyoanza 1996.

*kwendo58@gmail.com*

*- Imetafsiriwa na Charles Wasonga*

# Tumbojoto kuhusu pesa za mahasla

Kutoka 7

imetangaza kuunga mkono sekta ya biashara ndogo kama njia ya kutimiza mfumo wake wa kiuchumi wa 'Bottom Up', haijaruhusu uagizaji bidhaa "kwa wote bila malipo" isipokuwa kupitia mfumo rasmi wa ushuru na viwango sahihi vya ubora.

Hasa, kasi ambayo serikali imeonyesha katika kuongezea sehemu za kutoa ushuru inaashiria kuwa biashara maarufu, maarufu kama 'Uchumi wa Nyamakima', ambazo zimekuwa zikikwepa kulipa ushuru kwa miaka mingi sasa zitalazimika kulipa ushuru huo.

Kamau anasikitika kuwa muungano wake haukualikwa kuchangia wakati wa kubuniwa kwa kanuni za kudhibiti utekelezaji wa Hazina ya Hasla au mapendekezo tofauti ya ushuru ambayo yataathiri sekta hiyo.

"Hatuna matumaini makubwa kama tuliyokuwa nayo mwanzoni," ndiyo kauli yake kuhusu ahadi ya Kenya Kwanza ya 'Bottom Up'.

Kwa maoni yake, Hazina ya Hasla itafeli kama mipango mingine ya serikali za awali, masuala muhimu yasipotatuliwa. Anahofia kila mfanyabiashara akiruhusiwa kupata pesa hizo, zitakuwa sawa na zinazotolewa wakati wa kampeni na watu wengi watashindwa kulipa.

Badala yake, anapendekeza zitolewe kupitia vyama vya ushirika, vya wafanyabiashara na makundi mengine maalumu ambako mshikamano na uwajibikaji katika kulipa mikopo ni wa kiwango cha juu.

Serikali inafaa kurahisisha usajili wa makundi kama hayo, ili yawape wanachama mafunzo kuhusu hazina hiyo na pia yatumike kuombea mikopo.

*- Imetafsiriwa na Wanderi Kamau*

Nation Media Group "Digital Copy"

kurunzi ya kenya

KUKABILIANA NA ZAIDI YA MAKUNDI 150 YA WAASI NCHINI DRC

# HATUHITAJI UKUTA MPAKANI

**Katika mahojiano ya kina na 'Darubini ya Wiki', Waziri wa Ulinzi Duale anaelezea maono yake kuhusu kuimarisha KDF, vita dhidi ya Al-Shabaab Somalia, shughuli za jeshi nchini Congo na kutumiwa kwa jeshi katika serikali ya Uhuru**

NA OSCAR OBONYO

Unakumbuka ujenzi wa ukuta wa mawe wa kilomita 700 kwenye mpaka wa Kenya na Somalia kwa lengo la kurudisha amani katika mpaka huo na kuzuia wanachama wa kundi la kigaidi la Al-Shabaab? Sasa Waziri mpya wa Ulinzi, Aden Bare Duale, anataja hatua hiyo kuwa ya kizamani na anapanga kuanzisha mfumo mkubwa wa kisasa wa usalama.

Wazo la kujenga ukuta huo lilitokana na mashambulizi yaliyosababisha mauaji Kenya na kundi hilo lenye makao Somalia likiwemo shambulio katika Chuo Kikuu cha Garissa Aprili 2, 2015 ambapo watu 148 waliuawa. Ukuta huo ambao ulikuwa uwekwa kamera za usalama, waya wa seng'enge, ulinuiwa kuzuia magaidi hao wenye silaha kuvuka mpaka huo.

Katika mahojiano haya ya kwanza tangu alipochukua uongozi wa wizara hiyo muhimu, Duale pia anazungumzia mzozo wa muda mrefu kati ya Kenya na Uganda kuhusu Kisiwa cha Migingo, ambao umetajwa kwa mzaha na Rais wa Uganda Yoweri Museveni kuwa "vita visivyo na maana kuhusu kipande cha ardhi ya miamba katika Ziwa Victoria".

Katika mahojiano haya ya kipekee, Duale pia anajibu masuala tata ya kutumwa majuzi kwa Jeshi la Ulinzi la Kenya (KDF) katika mashariki ya Congo, kikosi kilicho Somalia, na jukumu linalomsubiri katika Makao Makuu ya Ulinzi. Yafuatayo ni mahojiano hayo:

***Bwana, tuanze na uteuzi wako. Kwa nini unafikiria Rais alikuteua kuwa Waziri wa Ulinzi? Je, una tajiriba au ufahamu katika masuala haya?***

Sijui ni kwa nini aliniteua kwa kuwa ni yeye tu anayeweza kuelezea ufaafu wangu. Hata hivyo, nitachukua wajibu huu mzito niliotwikwa na Rais kutekeleza majukumu yangu kwa bidii na kuridhisha inavyohitajika. Na isipokuwa kukutana na wanajeshi nikiwa shule ya upili, ambayo ni Moi Forces Academy nilikosomea Kidato cha Tano na Sita, na kwamba nimeoa binti ya Jenerali wa Jeshi, sina mafunzo au tajiriba ya kazi. Hata hivyo, niko sawa kabisa na wanajeshi na nitajaribu kuleta tofauti wakati wangu nikiwa Waziri wa Ulinzi.

***Wasomali Wakenya na walio Somalia, Ethiopia na maeneo mengine ya Upembe wa Afrika wanakuheshimu kama kiongozi maarufu katika ukanda huu, Utasawazishaje matarajio yao na yale ya raia wa nchi yako?***

Ni kweli kuwa mimi ni kiongozi maarufu miongoni mwa jamii za Wasomali na Waislamu Kenya na ukanda wa Upembe wa Afrika. Hata hivyo, kwanza mimi ni Mkenya na inayofuata ni kuwa mimi ni Msomali. Nimekuwa mbunge kwa mihula mitatu na nilishinda muhula wa nne na nimekuwa Kiongozi wa Wengi wa kwanza na aliyehudumu kwa muda mrefu katika Bunge la Kitaifa, sasa nataka kuacha alama katika serikali. Nataka kuongeza thamani katika serikali yangu.

***Na unafikiri kazi yako itakinzana na siasa za ukoo?***

Hili ni swali la kuudhi na lisilo haki ambalo nimekuwa nikiulizwa. Mimi ndiye Mkenya wa kwanza kutoka jamii inayopatikana kila mahali nchini kuteuliwa Waziri wa Ulinzi? Au tunamaanisha kuwa Wamaasai, Waluo, Wabukusu, Wakuria na wengine, hawafai kushikilia wadhifa huu? Na je, mimi ndiye Msomali wa kwanza kushikilia wadhifa wa Ulinzi au Usalama? Wengine walionitangulia kama Seneta Yussuf Haji, walifanya kazi yao na sidhani walishindwa na kazi au kuweka usalama wetu hatarini.

***Unapoanza kazi kuna malalamishi miongoni mwa Wakenya kuhusu "kutumiwa kwa wanajeshi katika huduma za serikali". Je, tunafaa kutarajia hayo katika serikali hii?***

Ilikuwa makosa kwa aliyekuwa Rais (Uhuru Kenyatta) kuwapa wanajeshi mamlaka ya kiraia, na kisingizio cha utendakazi mzuri wa KDF hakina msingi. Ingawa maafisa wangu wanaweza kufanya kazi nzuri, jukumu hilo linapaswa kutekelezwa na taasisi na wafanyakazi kulingana na katiba. Ugatuzi ni awamu muhimu katika Katiba yetu, na ndiyo sababu tunashikilia kuwa wazo la NMS (Nairobi Metropolitan Service), iliyoongozwa na afisa wa jeshi lilikuwa kosa kubwa. Hata wazo la kuhamisha kampuni ya nyama ya Kenya Meat Commission kwa jeshi halikufaa na kwa sasa tuko katika harakati za kubadilisha hayo yote. Naweza kukuhakikishia kuwa kuendelea mbele, Amiri Jeshi Mkuu wa KDF atarekebisha makosa kama hayo ya awali.

***Kando na hayo, una mawazo gani kuhusu mzozo wa muda mrefu kuhusu umiliki wa Kisiwa cha Migingo katika Ziwa Victoria?***

Suala hili linashughulikiwa, sio tu na wizara yangu lakini kuna zingine tatu - Usalama wa Ndani, Mashauri ya Kigeni na Ardhi. Mazungumzo yanaendelea katika viwango vya juu vya serikali zote mbili za Kenya



Waziri wa Ulinzi Aden Duale. DENNIS ONSONGO I NATION

Nation Media Group "Digital Copy"

## kurunzi ya kenya

na Uganda.

***Unasemaje kuhusu wavuvi wetu wanaonyanyaswa na kukamatwa kila wakati na maafisa wa Uganda?***

Kukamatwa kwa wavuvi wetu na pia suala la Migingo kunatokana na mzozo wa mpaka kwenye ziwa. Hili ni jambo muhimu kwetu na tunalenga kutatua mambo hayo mawili. Kwanza tutajaribu kusuluhisha mzozo wa mpaka, kupitia mawaziri wa nchi hizi mbili.

***Kutokana na kile Jenerali wa Jeshi la Uganda alisema juzi kwenye mitandao ya kijamii, uko tayari kutumia fursa hiyo - kwa kuwa sasa una mamlaka – kuonyesha majirani wetu kuwa sisi ni wenye nguvu katika eneo hili?***

Tuna uhusiano mwema na Uganda na tunamheshimu Rais Yoweri kama kiongozi na rafiki mkubwa wa nchi yetu na Rais. Hayo kando, suala hili tayari limeshughulikiwa katika viwango vya juu vya serikali na Rais Museveni akamuomba mwenzake msamaha. Ninachoweza kuongeza ni kuwa uwezo wetu wa kijeshi eneo hili ni wa hali ya juu na hili linajulikana na wote.

***Kuhusu nafasi yetu katika eneo hili, Ijumaa iliyopita, Rais William Ruto alituma wanajeshi zaidi ya 900 kukabili makundi yenye silaha katika mashariki ya Jamhuri ya Demokrasia ya Congo. Ni nini kilishawishi hatua hii?***

Kwanza, huo sio uamuzi wa Rais au wa nchi yetu. Hatua hiyo inafuatia azimio la viongozi wa serikali katika Jumuiya ya Afrika Mashariki, baada ya DRC kujiunga rasmi na muungano huo wa eneo Machi mwaka huu. Ni uamuzi uliofikiwa aliyekuwa rais akiwa mamlakani kwa lengo la kusuluhisha mzozo katika DRC. Mbali na Kenya ambayo inatuma kikosi kimoja, Uganda, Rwanda na Burundi zitakuwa na vikosi viwili, Sudan Kusini kikosi kimoja huku Tanzania ikiahidi kujiunga na shughuli hiyo baadaye.

***Je, ni nini hasa lengo la kushirikisha vikosi hivi vya eneo?***

Lengo la kikosi hicho ni wazi - kutekeleza uamuzi wa viongozi wa nchi wa kurudisha amani katika mashariki ya Congo, kufungua njia za kupeleka misaada ya binadamu ili maskini na makundi yaliyo hatarini yaweze kushughulikiwa na pia kutoa nafasi kwa suluhisho la kisiasa.

***Nchi yetu itafaidika vipi, Bwana Waziri?***

Tunafurahia kushiriki kwa sababu kadhaa, ikiwemo ukweli kuwa tunawekeza katika amani katika eneo hili, ambayo itatuletea manufaa makubwa. Usisahau kuwa Kenya inachukuliwa kuwa mpatanishi asiyeegemea upande wowote katika hali hii kwa sababu sisi ni nchi ya pekee isiyopakana na DRC. Jeshi letu pia linaaminiwa na kuheshimiwa na tunatumaini kutumia hili na pia tajiriba yetu, kuwa na wanajeshi wetu katika vikosi vya kudumisha amani kote ulimwenguni. Hii inaimarisha uwezo na nafasi ya kubadilishana habari.

Haufikiri kuwa kwa kuhusika moja kwa moja, Kenya inajiweka katika hatari ya kujipata kwenye mzozo uliopo kati ya Uganda na Rwanda?

Tunafahamu ukweli kuwa tunaweza kuvutwa kwenye vita vinavyohusu mataifa mengine ya eneo hili. Lakini tumeshauriana ipaswavyo, kuanzia hapa nyumbani ambako tulipata idhini kutoka Bunge kulingana na Ibara 240 (8) ya sheria zetu, kutoka kwa mkuu wetu wa majeshi hadi kwa kiwango cha rais, ili kuhakikisha kila kitu kiko sawa, na kuwa hatujipati katika makabiliano ya huko. Kabla ya kuwasili DRC, pia tulihakikisha tulipata idhini kutoka kwa mashirika yote husika, kuanzia jumuiya ya kanda, AU na pia Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa.

***Tutakuwa DRC kwa muda gani, au tunaweza kujipata katika hali ya Somalia ambako tuliingia 2011 tukitarajia kukamilisha operesheni ya usalama haraka lakini hadi leo tumekwama nchini humo?***

Ninajua hali katika DRC inaweza kuwa hata ngumu zaidi, ikilinganishwa na Somalia ambako kundi la kigaidi la Al-Shabaab ndilo linalengwa. Hata hivyo, katika DRC, tunakabili hata zaidi ya makundi 150 ya waasi wenye silaha. Lakini hatuna mipango ya kuwa Goma, ambako wanajeshi wa Kenya wako, kwa zaidi ya mwaka mmoja. Tunaelewa ukweli unaohusiana na fedha na gharama zingine za kikosi kama hiki.

***Katika kisa cha Somalia, je kuna mipango mipya ya serikali kuhusu kuwepo kwa KDF katika nchi hiyo?***

Hatuna kalenda mpya mpya ya wanajeshi wetu Somalia, ikizingatiwa kuwa wanajeshi wa KDF wanahudumu chini ya ATMIS (Kikosi cha Mpito cha Muungano wa Afrika Somalia) pamoja na TCCs wengine (nchi zinazotoa wanajeshi). Tutakuwa nchini humo kurudisha amani na tutaondoka Mogadishu hili litakapotimia. Hata hivyo, kuna mpango wa kuondoka, kuanzia na nchi zilizo na wanajeshi wengi, kama vile Uganda. Lakini tangu KDF ilipoingia Somalia, magaidi wa Al-Shabaab bado hawajashindwa. Kuhusika kwetu ni kuhusu usalama wa taifa na tunaamini tumepata ufanisi kiasi kwa kuwa idadi ya mashambulizi imepungua. Kuwepo kwa KDF na wanajeshi wengi pia kumesaidia kufanya SNA (Jeshi la Taifa la Somalia) kupata ujuzi wa kitaalamu na kujenga uwezo wake wa kukabiliana na vitisho vya makundi ya magaidi.

***Hili linanikumbusha... ni nini kilifanyika na ukuta wa mawe ambao serikali ilikuwa ikijenga kwenye mpaka wa Kenya na Somalia?***

Sina habari kuhusu unavyoendelea au ambapo umefikia. Lakini nitazuru Mandera hivi karibuni binafsi kutathmini hali yake.

***Katika enzi hizi, bado unaamini ukuta huu ndio jinsi bora ya kuimarisha usalama?***

Huu bila shaka ni mpango wa kizamani. Sasa tunatayarisha mbinu bora na ya kisasa pamoja na serikali ya Somalia kwa usaidizi wa washirika wengine wa maendeleo kuimarisha usalama mpakani, na pia kufungua vituo salama vya kupitia sehemu za Kiunga, Liboi na Mandera. Tumeweka miundomsingi inayohitajika upande wetu na tunasubiri Somalia kuweka yake. Hii itahusisha idara tofauti za wizara za Ulinzi, Usalama na Mashauri ya Kigeni. Mwishoni mwa mpango huu, tutahakikisha tutakuwa na mbinu bora ya usalama.

***Mbali na hayo, unachukuliwa kuwa mfuasi mkubwa wa aliyekuwa Rais wa Somalia, Mohamed Farmaajo. Hali itakuwaje sasa kutokana na ukweli kuwa unafanya kazi na mpinzani wake mkuu, Rais Hassan Sheikh Mohamud, katika shughuli zako rasmi na Somalia?***

Ingawa ni kweli kuwa kwa kiwango cha kibinafsi Farmaajo ni rafiki, nitakuwa nikifanya kazi na serikali iliyo mamlakani. Pia ninajuana na Rais Hassan na ametuonyesha ana nia njema ya kufanya kazi na serikali ya Rais William Ruto, na sisi pia tumemkumbatia. Kama serikali, hatuhusiki na masuala ya ndani ya nchi zingine. Tunashughulika nayo kwa njia ya urafiki na ujirani mwema.

***Tutarajie nini kutoka kwa uhusiano wako na Somalia?***

Tutamuunga mkono Rais Hassan na watu wa Somalia kuleta amani katika nchi yao na katika eneo hili jinsi tutafanya DRC, Ethiopia na ndani ya EAC na IGAD.


***Na mwisho, una malengo gani mahususi kwa KDF?***

Nataka kulenga kuinua maslahi ya wanajeshi wetu wanaume na wanawake, kupitia huduma bora za afya, nyumba, mafunzo, na pia kuhakikisha wanapata vifaa vya kisasa na silaha. Nitaunda pia heshima na kuwepo wa wanajeshi wetu katika eneo hili. Tunajivunia kudumisha amani katika eneo hili na tunataka kuendelea kufanya hivyo.


*--Imetafsiriwa na Benson Matheka*

Nation Media Group "Digital Copy"


# habari kwa picha



Amirijeshi Mkuu wa vikosi vya waasi Tigray, Jenerali Tadesse Worede (kushoto), na mkuu wa majeshi ya Ethiopia, Field Marshal Berhanu Jula (wa pili kulia), wakisalimiana na aliyekuwa Rais wa Nigeria Olusegun Obasanjo na aliyekuwa Rais wa Kenya Uhuru Kenyatta baada ya kutiwa saini kwa maamuzi ya Mkutano wa Makamanda Wakuu wa kutekeleza Makubaliano ya Kudumu ya Kusimamisha Uhasama kati ya serikali na Chama cha Ukombozi cha Tigray People's Front jijini Nairobi mnamo Novemba 12. PICHA | AFP



Picha iliyopigwa kwa kifaa jina James Webb Space Camera mnamo Novemba 16 kikionyesha aina ya nyota iliyopachikwa ndani ya wingu la nyenzo zinazosaidia ukuaji wake.PICHA | AFP



Mwakilishi wa kampuni ya Sotheby's jijini Hong Kong akishika almasi jijini Hong Kong mnamo Novemba 15. Almasi hiyo inatarajiwa kuuzwa kwa kiasi kisichopungua dola za Amerika 5 milioni (karibu Sh600 milioni) jijini Sotheby's Disemba ijayo. PICHA | AFP



Sehemu ambako shambulio la kombora liliua wanaume wawili katika kijiji cha Przewodow, mashariki mwa mpaka wa Poland, karibu na mpaka na Ukraine iliyoharibiwa na vita mnamo Novemba 15. PICHA | AFP



Kikosi cha polisi cha Ukraine cha kutegua mabomu kikikagua eneo la kituo cha kuhifadhia nafaka kilichotumiwa kama kituo cha kijeshi cha Urusi wakati wa uvamizi katika eneo la Snihurivka mnamo Novemba 16. PICHA | AFP



Watu wakusanyika katika eneo la Flag jijini Doha mnamo Novemba 15 kabla ya mashindano ya Kombe la Dunia Qatar 2022. PICHA | AFP




Aliyekuwa Rais wa Amerika Donald Trump akizungumza mjini Florida mnamo Novemba 15. Ametangaza kugombea urais kwa mara ya tatu, hatua inayotarajiwa kusababisha ushindani mkali katika uteuzi wa chama cha Republican baada ya matokeo mabaya ya wagombeaji alioteua yeye binafsi katika uchaguzi wa katikakati ya muhula. PICHA | AFP

Nation Media Group "Digital Copy"

Vija
Jukwaa L



# MALKIA WA HAKIMILIKI

*Aliyekuwa mshindi wa taji la malkia wa urembo katika chuo kikuu na wakili Liz Lenjo aliona pengo na akaamua kulijaza, hatua iliyompeleka kuongoza Mahakama ya Hakimiliki Kenya*

NAFASI YA VIJANA

## WANAVYOSEMA



**Benard Karanja**

Wakenya wanataka kuona hatua kali dhidi ya wahalifu. Badala ya polisi kuchapisha maeneo hatari, wanafaa kuongeza doria katika maeneo hayo. Tunaelekea msimu wa sherehe, ambapo Kenya inaonekana kuwa eneo moja kubwa la uhalifu. Serikali inafaa kuonyesha kujitolea kwake katika kukabili ukosefu wa usalama. Waziri wa Usalama wa Ndani Kithure Kindiki anafaa kuamuru msako mkali.

*-Kiongozi wa vijana na kiongozi wa zamani wa wanafunzi Chuo Kikuu cha Kenyatta*



**Tonny Olela**

Asilimia zaidi ya 50 ya wahalifu wote wanaotumikia vifungo vyao ni vijana wa umri wa kati ya miaka 16 na 25. Siku za hivi karibuni, usalama umezorota kutokana na idadi kubwa ya watu, utumiaji mihadarati, umaskini na ukosefu wa ajira. Kushuka kwa motisha wa kazi miongoni mwa polisi kutokana na kuhangaishwa kumefanya hali kuwa mbaya zaidi. Tengeneza nafasi za ajira miongoni mwa vijana na kuboresha mazingira ya kazi ya polisi.

*- Jopo la Ushauri wa Vijana, UNPF*



**Faith Jeruto**

Uhalifu umeoingezeka kote nchini, huku polisi wakionekana kutochukua hatua za kutosha kuukabili. Wengi wanaohusika ni vijana,wanaotaka kupata pesa za haraka. Serikali inafaa kuingilia kati na kutoa suluhisho kabla ya hali kuharibika zaidi. Vijana hao wanaweza kutoa mchango mkubwa katika sekta tofauti za kiuchumi wakipewa nafasi.

*- Mwanafunzi*



**Deon Wandera**

Uhalifu huongezeka hali za kijamii na kiuchumi zikidorora. Serikali pia ilikosea kuvunja Kikosi cha Huduma Maalumu cha Idara ya Upelelezi wa Jinai. Huenda kilikuwa na mapungufu yake lakini kilifanya kazi nzuri katika kukabili uhalifu. Kuhusu wizi wa mifugo, serikali inafaa kutafuta suluhisho la kudumu kwa suala hili.

*- Kiongozi wa Vijana, Democratic Action Party*

# WEWE NI HASLA? KAZI RASMI INAFAA ZAIDI

**Nchi zinazostawi:** Matatizo ya Kenya kwa kiasi kikubwa yanatokana na kuegemea zaidi uchumi usio rasmi

● NA WYCLIFFE OSABWA

Hazina ya Hasla, mradi mkubwa zaidi wa serikali ya Kenya Kwanza, unakaribia. Mradi huo unalenga kurahisisha kupatikana kwa mikopo, kuleta pamoja raia wa kiwango cha chini katika jamii na kuinua biashara ndogo zilizopo.

Kama nilisoma vizuri, serikali inajaribu kutimiza mambo mawili muhimu kwa wakati mmoja. Kwanza, inalenga kupanua sekta rasmi kwa kuwataka wote watakaofaidika na Hazina hiyo kusajili biashara zao. Pili, inajaribu kuwafadhili 'mahasla' ili kuwawezesha kutoka katika umaskini.



Matatizo yanayopatikana Kenya, sawa tu na nchi zingine zinazostawi kiuchumi, kwa kiasi kikubwa yanatokana na kuegemea zaidi uchumi usio rasmi. Hii ni hali ambapo watu na mashirika huficha mapato yao kutoka kwa serikali hivi kwamba haziwezi kujua kiasi cha mapato yao kwa lengo la kuyatoza ushuru.

Kinyume na hayo, uchumi rasmi unaruhusu ukusanyaji rahisi wa ushuru na unaoweza kutabiriwa, pamoja na ada nyingine kama NHIF na NSSF. Hili ni muhimu, kwani hakuna serikali inayoweza kujisimamia bila makusanyo kama hayo.

Hatua zozote inazochukua serikali, lazima ikumbuke kuwa sekta isiyo rasmi ya Uchumi hustawi kutokana na udhaifu wa sekta rasmi. Baadhi ya watu hujiunga na sekta isiyo rasmi baada ya kupoteza kazi zao. Wengine hufanya hivyo kwa hiari yao ili kuepuka changamoto walizokumbana nazo katika sekta rasmi, kwa mfano, kiwango cha juu cha ushuru. Je, hili linatukumbusha jambo fulani?

Katika nchi za Afrika ya Kusini mwa Jangwa la Sahara, inakisiwa uchumi usio rasmi unajumuisha asilimia 70 ya jumla ya idadi ya watu. Kati yao, asilimia 90 wanaweza tu kumudu majukumu yasiyohitaji taaluma kwa sababu hawana ardhi, mtaji wa kifedha au teknolojia.

Jambo linalonifanya nipendekeze kuwa Hazina ya Hasla inafaa zaidi kwa walio katika biashara rasmi ili waweze kupanua na kujumuisha mahasla wanaoishi maisha ya kupata leo wasijue kesho itakuwaje. Kwa kutumia nadharia za kiuchumi, anahitaji kuelewa maisha ya watu hao, na hali ya uchumi. Tuna watu ambao wamezoea kazi za mishahara na wanaoepuka kulipa ushuru wanapojiajiri. Kupanua nafasi katika uchumi rasmi ni njia rahisi ya kuwanasa, ili kuongeza kiwango cha watu wanaotozwa ushuru. Isitoshe, mahitaji ya dharura ya 'mahasla' wengi hayawezi kutimizwa kwa mkopo wa mara moja, ambao, kama hautatumika mara moja, utaishia mikononi mwao katika biashara za kubahatisha. Sitataja wanaokopa bila kukusudia kulipa, na makundi ya kujisaidia yanayovunjika haraka kuliko yalivyobuniwa.

Kubuniwa kwa uchumi rasmi kunahitaji mkakati madhubuti. Kwa mataifa yanayostawi, unatekelezwa vizuri zaidi kwa kuruhusu ukuaji wa biashara rasmi zilizopo. Leo, biashara nyingi bado zinapitia changamoto za kifedha kutokana na athari za janga la Covid-19. Ingekuwa vizuri kufadhili biashara zilizopo, biashara za kiteknolojia na zile zinazoanza.

Zaidi ya hayo, changamoto zinazosukuma biashara rasmi katika sekta isiyo rasmi ya kiuchumi, kwa mfano masharti mengi ya kisheria na uzingatiaji wa kanuni nyingi za ushuru, zinapaswa kushughulikiwa. Kuna watu wengi wanaoendesha biashara zenye faida nyingi kwa njia zisizo rasmi lakini hawatozwi ushuru. Na wengi huendesha shughuli zao kisiri, hivyo, chini ya kiwango kinachohitajika, kwa kuhofia kukabiliwa kisheria. Hata kama serikali itatuma watu wengi kuhakikisha ushuru unalipwa, itakuwa ikitumia pesa hizo kuwalipa, bila kuzingatia hongo zitakazotolewa katikati mwa shughuli hizo.

Serikali izingatie kukuza uchumi rasmi, hata kama itachukua muda mrefu. Waafrika huhamia ugenini kwa sababu zina chumi rasmi zinazoweza kuwajumuisha.

*Bw Osabwa ni mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Alupe, Busia. Una majibu yoyote kuhusu masuala yanayoibuka? Tungependa kusikia kutoka kwako. Tuma maoni yako kwa:*

***weeklyreview@ke.nationmedia.com***

*- Imetafsiriwa na Wanderi Kamau*

Nation Media Group "Digital Copy"

MTAZAMO WANGU



# KOMBE: MCHEZO MARIDADI

**Lugha ya wengi katika spoti:** Ndiyo hafla kubwa zaidi kuwahi kubuniwa. Inachanganya utaifa, nguvu na ushindani kuhusu ni nchi gani bora

• NA WAGA ODONGO

Kandanda ndiyo lugha ya wengi duniani; sote tunaifahamu na tunaizungumza. Waamerika wanajifanya hawaipendi, kandanda yao ni aina ya mchezo wa raga wenye magwanda ya kukinga mabega, lakini wanapenda. Huko, soka ni mchezo wa wanawake.

Timu ya Taifa ya Wanawake imeshinda medali nne za dhahabu na idadi sawa ya makombe ya dunia. Timu ya wanaume ikifanya vyema itaungana na wenzao wa kike.

Ufanisi katika kandanda ya dunia unatokana na changamoto iliyopo, ukihusu miguu miwili, na kutimua mbio huku wengine wakikufuata na wakati huo ukidhibiti kitu kwa kutumia miguu yako tu. Michezo inayotumia mikono inaonekana kuwa hadaa ya aina fulani. Tuna uwezo wa kutumia vidole vyetu kwa hivyo kila kitu kinachohusu mikono yako huwa rahisi. Kandanda huwa ngumu kutokana na ustadi unaotumika lakini pia ni rahisi kwa wengi kujaribu. Kila mvulana kila mahali amewahi kuingiwa na fikra mbili wakati fulani: naweza kurusha jiwe hili umbali gani, na ninaweza kupiga mpira huu hadi umbali gani. Ni fikra za kimaumbile, ndio mchezo chaguo la wengi duniani.

Kombe la Dunia, kwa hivyo, ndilo tukio kubwa kuwahi kubuniwa. Inachanganya utaifa, nguvu na ni ushindani unaoendelea kuhusu ni nchini gani bora. Shindano ambapo nchi tofauti hupata nafasi ya kuonyesha ushindani wake.

Ukishinda utakuwa na haki ya kujivuna kwa miaka minne. Nani anaweza kusahau Wasenegal walipowanyuka waliokuwa watawala wao wa kikoloni mnamo 2002?

Fainali za mchezo huo pia zina kumbukumbu. Nani anaweza kusahau wendawazimu wa Zidane dhidi ya Materazzi? Kama angevumilia kwa dakika chache zaidi na kufikia mikwaju ya penalty...

Kombe la Dunia ni maarufu zaidi kiasi kwamba shirikisho la kandanda ulimwenguni, Fifa, lina wanachama 211 wanaojaribu kufuzu kwa mchuano huo ilhali Umoja wa Mataifa (UN) una wanachama 193 pekee. Linavutia mataifa kujiondoa katika ndoa za kisiasa na badala yake kutafuta utukufu wa spoti. Uingereza huvunja Sheria yake ya Muungano na Scotland kuhakikisha mataifa yote manne ndani yake yanaingia uwanjani. Ni sawa kutumia sarafu moja, Bunge na kuwa chini ya utawala wa mfalme lakini kilicho muhimu kwa watu wa Scotland ni kuwashinda walinzi wao wa Uingereza katika kandanda ya kimataifa.

Shida hata hivyo ni kuwa mwenyeji wa Kombe la Dunia. Maandalizi ya shindano hilo yamekuwa sherehe ya kutetea masilahi ya utaifa. Kandanda siku hizi ni uwanja wa mashindano ya ubabe kati ya mataifa na ni vita bila bunduki. Ugonjwa huo hasa umeenea Mashariki ya Kati. Qatar ilinunua timu ya PSG na kuleta pamoja wachezaji wenye talanta ambazo hazijawahi kuonekana katika timu moja. Nchini iliyokuwa kizuizi kwao miaka michache iliyopita, Saudi Arabia, ilinunua Newcastle na inaendelea kufanya hivyo. Wakati huo huo, Abu Dhabi ina Manchester City, mabingwa wa Uingereza katika miaka minne kati ya mitano iliyopita. Ili kuwa klabu ya juu Uropa nyakati hizi unahitaji kuwa tawi la spoti la taifa kuu lenye utajiri wa mafuta. Kitu kimoja ambacho unapaswa kuwa na hakika nacho ni kuwa, iwapo vikwazo dhidi ya Iran vitaondolewa leo, viongozi wan chi hiyo wataandaa mkutano na wanahabari na kulaani Ubeberu wa Amerika, kukashifu Magharibi kwa uozo wake na kutangaza kununua Manchester United kwa matumaini ya kuwashinda City na Newcastle.



Maandalizi ya shindano lenyewe yamekuwa ghali kiasi kwamba ni walio na bajeti kubwa ya kutumia ndio wanaotafuta nafasi hiyo. Kombe la Dunia na dada yake wa kambo, Olimpiki, yanajulikana kwa kufilisisha miji mikuu; nchini Brazil, yalichangia kuharibiwa kwa mitaa duni na kuhamishwa kwa maskini ilhali Ugiriki ilifilisika na bado inahisi madhara ya kuandaa Michezo ya Athens. Mashindano hayo husababisha miradi mingi isiyo na manufaa na ufukara nchini.

Hata kwa viwango vya ubadhirifu vya Kombe la Dunia, lile la Qatar limefikia kiwango kipya cha juu. Nchi itatumia pesa nyingi ili iweze kukalika, zikiwemo ndege za kuzalisha mawingu angani, mitambo ya kutoa hewa safi yenye ukubwa wa milima na nyumba za malazi ambazo zimejengwa upya. Gharama ambayo itakuwa zaidi ya Dola za Amerika 200 bilioni (karibu Sh2.4 trilioni), inaweza kugharamia matibabu ya nusu ya magonjwa duniani. Fifa kama shirikisho linaonekana kuchuma pesa nyingi kutoka kwa viongozi wa mataifa wenyeji wanaotafuta umaarufu kutoka kwa halaiki kubwa ya watu.

Shirikisho hilo huendesha shughuli zake kama genge la wahalifu kuliko asasi ya spoti kufuatia madai ya utoaji hongo yanayokumba kila shindano.

Qatar ni nchi tajiri kwa njia isiyo ya kawaida, ikikalia bahari ya mafuta wakati ambao ulimwengu unayahitaji. Inamudu kuandaa michezo lakini michezi ya 2022 inajiri wakati ambao wahamiaji wanahangaika kwa kunyanyaswa.

Shida pia ni hisia kuwa nchini nyingine itakayoandaa shindano hilo inafaa kuwa chonjo. Shindano la sasa linaongezea orodha ya matukio ya hivi karibuni katika mataifa tajiri ambayo yana rekodi isiyo nzuri ya haki za kibinadamu. Hata Saudi Arabia, taifa la kipekee lisilo na mto, ni mwandalizi wa Michezo ya Olimpiki ya Msimu wa Baridi Asia, 2029. Huenda Kombe la Dunia pia likaandaliwa Riyadh hivi karibuni. Kandanda inafaa kuhusu mashindano na sio jukwaa la mvutano miongoni mwa watawala. Kazi ya kuandaa Kombe la Dunia huenda inahitaja kutengewa nchi chache za Uropa ambazo tayari zina miundomsingi na viwanja vya kutumia.

Tayari shindano hilo ni la Uropa huku mialiko ya kushiriki ikutumwa kote duniani. Ni timu kutoka bara hilo pekee zilizo na nafasi ya kushinda. Mabingwa wanne wa mashindano yaliyopita wanatoka Uropa. Hata nyakati chache ambazo Amerika Kusini imeshinda imesaidiwa na wachezaji wanaocheza na kuishi Uropa. Dunia haiwezi kugharamia kundi la wasafiri kwa mchezo huu mzuri.

*Bw Odongo ni Mhandisi wa Kompyuta*
***wagaodongo@gmail.com***

*- Imetafsiriwa na Charles Wasonga*

Nation Media Group "Digital Copy"

HAKI ZA MALI ZA KIAKILI

# SURA, AKILI NA SHERIA YA HAKIMILIKI

**MALKIA WA UREMBO WA CHUO KIKUU:** Akiwa mwanafunzi, Liz Lenjo aliona pengo la uwakilishi wa kisheria kuhusu haki za picha na akaamua kulijaza, hatua iliyompeleka kuongoza Mahakama ya Hakimiliki Kenya

• NA EDDY ASHIOYA

Kama sura zinahadaa, basi nimehadaiwa vya kutosha na Elizabeth 'Liz' Lenjo, ambaye ana urefu wa futi tano inchi moja, ilhali anaonekana sawa na Robert Wadlow, ambaye ni bingwa katika kitabu cha wanaoweka rekodi na maajabu duniani cha Guinness. Rekodi hiyo pia ionyeshe kuwa mazungumzo yetu, ingwa yanafurahisha, yanafanywa wakati wa wingu la huzuni.

Kifo na hasara zinasikiliza mazungumzo yetu, kama mdudu katika ukuta anayesikia mengi bila kutambuliwa.

Ni karibu mwezi mmoja tangu Liz Lenjo amzike baba yake, na hauhitaji kuwa mtu mwenye huruma kuhisi mfadhaiko alionao, uchungu unaonekana wazi. Tuko Sarit Center, na anakumbuka aliposafiri Amerika kusherehekea na baba yake, baada ya kuteuliwa mkuu wa Baraza la Mahakama ya Hakimiliki.

Kisa cha kuwa karibu sana na kitu ilhali haukipati. Ananiambia haya na ninaona kifo changu machoni mwangu, yote ni ubatili, lakini hamu ni ya kubaki kuishi. Alihama Nairobi, na sasa anaishi Malindi, kwa miaka minne iliyopita, na mara kwa mara, japo nadra sana, hutembea Nairobi.

"Sana sana kwa mikutano ya kikazi." Kwa maana nyingine, ukitaka kuzungumza naye, nenda aliko, jambo ambalo sio baya inavyosikika. Ukizungumza naye, unabaini kuwa unaweza kuwa umefaulu sana.

Amekuwa mwigizaji, mwanamitindo, mwimbaji na wakili. Yake ni kama hadithi ya Cinderella: msichana asiyejulikana anayewatazama wengine na kujiuliza kwa nini wawe hivyo? Mbona nisiwe kama wao?

Kama marehemu baba yake, Liz ni mtu anayejitolea kwa kila afanyacho, kwa moyo wake wote. Wa kwanza kufika, na wa mwisho kuondoka. Kwa hivyo tuanzie wapi? Alianza vipi? "Nilipokuwa nikikua, nilitaka kuwa mwanamuziki. Nilitaka kuwa kama Michael Jackson. Wazazi wangu hawakuniunga mkono na nikalazimika kutafuta 'kazi' nyingine ya maana."

Akiwa mmoja wa wanafunzi wa kwanza wa sheria katika Chuo Kikuu cha Catholic University of East Africa, Liz alikuwa mhariri wa jarida la chuo hicho (Campus Vybe). Awali, alikuwa gumzo chuoni humo baada ya kunyakua taji la Miss Catholic University. Urefu wake ni futi 5 na inchi moja. Pengine mmoja wa wanamitindo wafupi sana katika historia ya Kenya. Kuanzia hapo, alikuwa nyota iliyopaa na kuangaza mbali.

Alijipata vipi katika sheria ya hakimiliki? "Nilikuwa napamba jarida la shule, na wakaambatisha picha yangu na chapa ambayo sikutaka kuhusishwa nayo. Kupata wakili wa kuniwakilisha ilikuwa vigumu kwa kuwa watu (wengi) hawakufahamu haki za picha zilikuwa nini (wakati picha yako inatumiwa bila idhini yako). Kwa hivyo, niliona pengo na nikalijaza."

Wakati huo, alikuwa katika kundi dogo, bado akilenga kuwa kama Michael Jackson. Hizo zilikuwa enzi za makundi ya wavulana na wasichana. Fikiria makundi kama Tattus na Semas. Alikuwa pia akiigiza katika sinema huku akiendeleza uanamitindo na kuandika. Ni alipokuwa akihoji wasanii maarufu ambapo aligundua wengi wao hawakuwa wakitumia mawakili katika majadiliano yao ya kandarasi. Alibaini watu hawakuwa wakitumia kandarasi au mawakili.

Mnong'ono ulipenya masikio yake, na maudhui ya mnong'ono huo yalikuwa: Naweza kufanya hili. Nitaweza kwa vyovyote. Na kuweza, aliweza. Alianza blogu mnamo 2010, na ikafaulu. Ili kupenya katika soko, aliwakilisha watu bila malipo. Alikuwa akiwakilisha yeyote. "Nilikuwa na kusudi na hilo lilinipa nafasi za kazi nyingine."

June Gachui, wakili mwingine mwimbaji, alimpa mmoja wa miradi mikubwa ya kazi yake (kufikia sasa), Makala ya Kwanza ya Coke Studio. Hii ilikuwa miezi michache baada ya Liz kuchukua likizo kutoka Chuo wa Uanasheria Kenya kujifungua mtoto wa kwanza. "Kazi yangu ilikuwa kupata leseni kutoka kwa wamiliki wa haki za muziki." Kazi ilikuwa ni kutafuta ni nani mwandishi wa wimbo? Ni nani aliye na haki za kuutayarisha? Kitu kingine, anamiliki kampuni ya bidhaa za urembo (MYIP Legal Studios, akiwa wakili wa kuilinda ili mambo yasiende kombo au kuanza kwenda kombo) na kama Drake anaweza kukufanya uamini, 'tulianzia chini hadi tulipo sasa.'

Ni kitu gani kilichobadilika tangu alipochukua usukani? Sidhani kuna mabadiliko mengi. Nafikiri haki inafaa kupatikana kila wakati na ukiwa kiongozi unafaa kuwa ukipatikana. Ninafanya kila niwezalo nisibadilike na kubaki nilivyo tu na kusimamia ninachoamini. Naheshimu kila mtu. Vyeo huja na kuondoka." Sasa, kila mtu humuita 'Bibiye Mwenyekiti.'



Elizabeth Lenjo ni mtaalamu wa sheria ya hakimiliki. PICHA | EDDY ASHIOYA

Nation Media Group "Digital Copy"

Milango yote iko wazi. Kimya cha heshima kinatanda. Hivyo ndivyo mamlaka hufanya, hivi kwamba unaweza hata kukishika.

Baraza la mahakama, anasema, ni mahakama spesheli. "Hatufanyi kazi kila wakati, ni kama mahakama kutafuta wataalamu kuisaidia kutoa haki. Kumaanisha bado tuko na muda wa kufanya mambo yetu mengine." Hata hivyo, anatoka kazini Ijumaa, adhuhuri. "Msimamo wangu ni kuwa ninafanya kazi kuishi lakini sio kuishi kufanya kazi." Hii ndiyo moja ya sababu zilizomfanya kuhamia Malindi. Ufanisi wake mkubwa umekuwa ni kupata digrii ya Uzamili katika mojawapo la masomo yenye ushindani mkubwa duniani. "Ilikuwa 2016, nilikuwa mwanafunzi wa pili wa kibinafsi kujiunga na mpango huo wa masomo (Sheria katika Hakimiliki kutoka Chuo Kikuu cha Turin, Italia) na Shirika la Hakimiliki Duniani (WIPO). Mpango wa masomo wa Turin ndio wenye ushindani mkalia zaidi kote duniani, na huwa wanasajili wanafunzi 40 kutoka kote duniani. Arobaini. Kati ya wagapi? Watu bilioni saba? "Nilikuwa najifunza kutoka kwa mababu wa IP."

Akiwa huko, alijiunga na kampuni ya mawakili jijini Las Vegas. Ni katika kampuni hiyo ambapo alijifunza thamani ya uaminifu, naam, nitakutetea lakini pia nitakukosoa. "Kuona wakili mwaminifu kiasi hiki ni ajabu." Kwa sababu katika ulimwenguni wa sasa usioona mbali, ukweli ni kilichoandikwa tu, sio kinachothibitishwa kuwa ukweli.

Mwaka mmoja baadaye aliteuliwa mwanachama wa bodi ya mahakama ya hakimiliki. Ni katika vikao vya kusikiliza kesi katika mahakama hiyo ambapo, Liz, akihitajika kuwepo ili kutimiza idadi inayotakiwa huku akimbeba mtoto wake mchanga mikononi na kuandamana na mumewe, mwanablogu wa teknolijia Al-Kags, alibaini kuwa huenda mumewe alikuwa nabii. Alimwambia, "Siku moja utakuwa mwenyekiti wa bodi hii." Maneno yake yalikuwa ya kinabii kweli, na jinsi waume wengi wanavyofahamu, ukipata fursa ya kuwa karibu na mumeo, unafanya hivyo kwa ujasiri. Kwa hivyo, alipoteuliwa mwenyekiti wa bodi ya mahakama ya hakimiliki, maneno yake ya kwanza, yalikuwa: "Nilikwambia!"

Akiwa mmoja wa wenyekiti wa baraza la mahama hiyo mwenye umri mdogo, siku za usoni zinaweza kuwa nzuri zaidi. Mama huyo wa watoto wawili pia anahudumu kama mwanachama huru wa bodi ya Shirika la Kawi ya Nuklia na Nishati ya Kenya, akitoa ushauri kuhusu masuala ya hakimiliki na usimamizi wa kampuni. "Siku moja kawi ya nuklia itakoma kueleweka vibaya. Najifunza mengi kuihusu."

Pengine kwake uongozi unamjia kwa urahisi. "Sitasema ni rahisi lakini ni kitu ambacho kimekuwa ndani yangu. Nikipewa nafasi naweza kufanya kitu, nitakifanya tu. Nilikuwa kiranja wa darasa (ilikuwa kazi ngumu), kisha nikawa mwakilishi wa darasa katika Shule ya Wasichana ya State House (ilikuwa bora kuliko ya kiranja, anasema); na nikiwa Chuo Kikuu nilitaka kuwa zaidi ya mrembo," Huenda uongozi haukumjia kwa urahisi lakini huwezi ukajua, kutokana na urahisi ambao anashikilia nyadhifa hizi. "Napenda maendeleo na kuendelea. Nataka kujua ninakoelekea." Moja la mambo anayopenda ni ulezi, ambao pia anafunza na kulea wanafunzi katika idara ya sheria ya Chuo Kikuu cha Strathmore.

Anajidanganya kuhusu kitu gani? "Nilidhani 'inawezekana' ni uongo hadi inapowezekana. Huwezi kujua unaweza kufanya kitu hadi unapokifanya." Kwa hivyo kifanye. Chochote unachotaka kufanya.

Anazungumza jinsi marehemu baba yake alikuwa akitania kwamba mawakili hawajui hesabu. Je yeye hajui hesabu? "Unaweza kujaribu hadi unafaulu." Naam, hiyo ni njia moja ya kujibu. "Unachohitaji ni kuwa na malengo."

Kuwa na malengo ndiyo ilikuwa kauli mbiu ya marehemu baba yake. Anazungumzia alivyompenda, mwanamume aliyekuwa nguzo katika maisha yake. "Ninahuzunika kwamba sikumwambia alivyokuwa muhimu kwangu. Nilidhani alijua tu." Je, ni vigumu kuwa kama yeye? "Unaona hii kazi ya kujitolea ninayofanya, nilijifunza kutoka kwake. Alikuwa mkarimu sana, mtu wa kutoa. Hatukujua alivyokuwa mkarimu hadi alipokufa. Alikuwa mnyenyekevu wa kupigwa mfano." Analengwalengwa na machozi machoni. Tunazungumzia wakati ambao maisha yamekuwa machungu kwake. Kifo kinakumbusha mtu kila kitu - nyakati za mapenzi, shughuli za maisha, kumbukumbu zinazoadhibu na kuinua. Kifo ingwa ni kitu cha kawaida kwa kila mtu kinagusa mtu binafsi. Hakijali kama wewe ni mtu maarufu au haujulikani sana na umma, kifo kinaumiza mtu binafsi na huleta kipindi cha huzuni. Alimpenda baba yake. Je, baba yake angesema nini kama angekuwa hai wakati huu? "Angesema ananionea fahari na kwamba nilizidi matarajio yake. Nilitia bidii sana."



## ALIYOKAMILISHA

Liz Lenjo ni mtaalamu wa sheria ya Hakimiliki, Burudani, Habari na Mitindo. Amefunza serikali kadhaa kuhusu Ufahamu wa Utamaduni na Desturi zikiwemo za Kenya, Bhutan na Ukanda wa Arctic.

Baraza la Mahakama ya Hakimiliki lilianzishwa chini ya sehemu ya 48 ya Sheria ya Hakimiliki ya Kenya (CAP 130).

Anahudumu katika Baraza la Mitindo ya Kenya kama Mkuu wa Hakimiliki na Sera katika Kamati ya Sheria. Ni mhadhiri katika Idara ya Sheria ya Chuo Kikuu cha Strathmore anakofunza sheria ya Uanahabari na Burudani na Sheria ya Biashara.

Liz ana digrii ya Uzamili (LL.M) katika Sheria ya Hakimiliki kutoka Chuo Kikuu cha Turin (Italia) na Shirika la Hakimiliki Ulimwenguni (WIPO), Digrii ya Sheria (LLB) kutoka Chuo Kikuu cha Catholic University of East Africa (CUEA) na Diploma ya Sheria kutoka Chuo cha Uanasheria cha Kenya.

Pia ana Cheti cha Sheria ya Mitindo kutoka Taasisi ya Sheria ya Mitindo - Chuo Kikuu cha Sheria cha Fordham (New York). Vile vile ana vyeti katika Usimamizi wa Hakimiliki, Upatanishi na Maridhiano kutoka Taasisi ya WIPO na mwalimu wa CopyrightX kutoka HarvardX.

Mnamo 2018, aliteuliwa na gazeti la Business Daily mmoja wa Wanawake 40 Maarufu wenye umri wa chini ya miaka 40.

Funzo kubwa analopata sasa ni jinsi ya kukubali mambo ya wengine. Mama yake, anasema, alikuwa kiranja mkuu wa familia. Akiwa kifungua mimba aliyefunzwa kudumisha nidhamu, anajifunza kukubali maoni tofauti ya watu wengine na kuyaelewa, akiwa mwangalifu - lakini akiheshimu haki ya kila mtu.

"Huwezi kufurahisha kila mtu. Kwa hivyo utafanya nini mkitofautiana?" Lazima ujue wakati wa kukaa ngumu na wakati wa kulegeza msimamo. Hii ni misingi miwili anayotumia kufanya maamuzi. Ananiambia kuwa kwa wakati huu anaogopa kifo. "Kukosa kufahamisha watu jinsi walivyo muhimu kwangu, ni kitu cha ukweli kabisa kwangu." Tunafikiri tuko na wakati, lakini hatuna. "Unajua bado ninapata simu za 'kunipongeza!' na 'Pole kwa kifo cha baba yako - zote kwa wakati mmoja."

Je, kuna mazuri katika yote hayo mazito? "Ndiyo nina watu wazuri karibu name wanaonisaidia. Kuanzia mama yangu na ndugu zangu na hasa mume wangu. Niliolewa na mume mzuri. Naam, nilipata mume mzuri kweli." Anamsifu mumewe, na inanikumbusha maumivu ya binadamu ya kupenda. "Alinisaidia kutimiza ndoto yangu." Sasa anafurahia kutimiza ndoto yake na anajua ufanisi unakuja, na atajua kwa sauti yake.

"Ninaposikia watu wakiniambia wanavutiwa na kupenda kuwa kama mimi, najua nimefaulu. Na nyadhifa nilizoteuliwa kushikilia pia zinaonyesha hivyo." Kama huwezi kufurahia vitu vidogo kwanza, basi hatutawahi vitu vikubwa.

Kujitoa mhanga ndiyo gharama ya kufaulu kwake. Alikosa muda wa kuwa na kufurahia na familia. Lakini ni lazima kila mtu apate haki yake, mpe Kaisari kilicho cha Kaisari. "Nimekuwa na bahati na mwerevu, sio tu kwa vitabu lakini katika maisha. Katika bahati, unatengeneza bahati yako kwa kile unachopatia ulimwengu." Akiwa na umri wa miaka 36, amezidisha matarajio yake.

Uko katika msimu gani wa maisha yako kwa wakati huu? "Niko katika mpito. Ninakumbatia uongozi; huu ndio msimu mkubwa. Baba yangu alisema ninaweza kufaulu, na nitafaulu," Kama shabiki mkubwa wa Michael Jackson, ni wimbo gani unaweza kuelezea maisha yake kwa mukhutasari? ". "You wanna be starting something. Huo na Try Again' wa Aaaliyah. Ah, nakwambia, baada ya MJ kuna Aaliyah." Ninaangalia wimbo wa Aaliyah tena, "Na usipofaulu mara ya kwanza (hufaulu mara ya kwanza) basi inuka na ujaribu tena Unaweza kujipanguza vumbi na kujaribu tena, jaribu tena."

*eddieashioya@gmail.com*

*- Imetafsiriwa na Benson Matheka*

Nation Media Group "Digital Copy"

MASOKO YA PESA

# MIKOPO YA RAHISI KWA FAIDA KUBWA

**FEDHA:** Mark Irungu alianza kuwapa mikopo marafiki walioishiwa na pesa kabla ya siku ya malipo kufika na kugeuza wazo hilo kuwa biashara ya kukopesha pesa yenye faida

• NA AMINA WAKO

Msanidi programu za kompyuta Martin Irungu alipoanza kuwakopesha pesa marafiki walioishiwa kwa ada kidogo mnamo 2010, labda hakujua wazo jinsi wazo hilo lingempeleka mbali. Leo, Irungu, 36, ndiye mwanzilishi wa PD Fund, kampuni ya kukopesha pesa iliyoanza shughuli zake rasmi mnamo 2016.

"Tuliungana tukiwa watu watatu na kukusanya Sh32,000 kama mtaji wa kwanza kwa biashara yetu ya kutoa mikopo baada ya kubaini kuwa marafiki wetu walihitaji pesa kabla ya siku zao za kulipwa kufika," akasema Irungu. Hata hivyo, miezi michache baada ya kuanza biashara hiyo watatu hao walikuwa 'wamekula' pesa zao zote na faida, na biashara hiyo ikaanguka.

Mnamo 2013, Irungu na marafiki wake wawili walipata tenda ya kusambaza jezi 8,000 kwa Halmashauri ya Ushuru Kenya (KRA) kwa maadhimisho ya wiki ya mlipa ushuru.

"Tulikuwa watu wa kwanza kufaidika kwa tenda zilizotengewa vijana na wanawake kupitia Mpango wa Uwazi wa Utoaji wa Tenda za Serikali (AGPO)," akasema.

Akiwa na nakala iliyoonyesha bei na kiwango cha jezi zilizohitajika na KRA (LPO), Irungu na marafiki wake walienda katika benki kadhaa wakitafuta fedha za kujaza tenda hiyo. (Nakala ya LPO husaidia biashara kupata fedha kutoka benki kulingana na kiwango cha tenda hiyo au barua za kuwasilisha bidhaa na huduma au kazi za kandarasi).

"Tulijaribu kushawishi benki kufadhili tenda yetu lakini zilitaka dhamana; zilisema tukifanikiwa kwenye tenda hiyo na kufaulu kulipwa, zingefadhili tenda iliyofuata," akakumbuka Irungu. Mwishowe, marafiki hao watatu walipeleka vitabu vya umiliki wa magari yao kwa wakopeshaji ili kupata pesa za kutekeleza tenda hiyo.

Walifaulu kuwasilisha jezi hizo, lakini iliwalazimu kungoja kwa siku 90 ili kulipwa. "Tulipokuwa tukingoja pesa zetu, riba ya mikopo yetu ilikuwa ikiongezeka," akasema Irungu. "Kufikia wakati wa kulipwa pesa zetu, tulitumia sehemu kubwa kulipia mikopo hiyo."

Walipata tenda zaidi kuwasilisha jezi na bahasha, lakini mapato, hasa kutokana na bahasha, yalikuwa kidogo.

Masaibu waliyopitia yalimuacha Irungu akifikiria iwapo kuna njia ambayo wafanyabiashara wanaweza kupata mikopo ya haraka na isiyo na kiwango cha juu cha riba. Alipokuwa akiwaza kuhusu hilo, alitoka katika shirika la InterNews-Kenya kwa kazi nzuri katika taasisi inayohudumu kote barani Afrika.

Akiwa bado mchanga, bila familia na akiendelea kupata tenda, Irungu alitunza mshahara wake vizuri, jambo lililomwezesha kupata mkopo mkubwa. "Nilipakua kandarasi yangu ya kwanza kutoka kwa mtandao na kuilainisha. Sikuwa na jina la biashara; ilikuwa isiyo rasmi sana lakini ilifaulu." Aligundua wateja wake wengi walikuwa watu walioajiriwa. Mnamo 2016, alisajili Kampuni ya Utoaji Mikopo ya PD Fund na kuamua kufanya kazi na mashirika tofauti ili awe akitoa mikopo kwa wafanyakazi wake.

"Unapoomba malipo ya mapema ya mshahara katikati ya mwezi, unavuruga shughuli za kampuni kwa kubuni migongano ya kifedha. Kwa hivyo nilifikiria, naweza kubuni ushirika na kampuni tofauti ili wafanyakazi wake wakitaka mishahara ya mapema wanawatuma kwetu?" Marafiki wake walikusanya pesa kumsaidia kutimiza kiwango kikubwa kilichohitajika.

Miaka saba baada ya kuanza biashara ya PD Fund, Irungu anaitaja kuwa safari ya kujifunza iliyojawa na changamoto. "Changamo-



**Afisa Mkuu wa Mikakati wa PD Fund, Mark Irungu, akihojiwa katika ofisi za kampuni hiyo eneo la Gigiri, Nairobi, mnamo Septemba 30.** PICHA | FRANCIS NDERITU

Nation Media Group "Digital Copy"

> **Changamoto yetu kubwa ilikuwa kubuni mfumo wa kujua anayefaa kupewa pesa. Pili ni jinsi ya kupata pesa zetu kutoka kwa wasiolipa, lakini Mahakama ya Madeni Madogo imetusaidia sana, kwani kesi moja huchukua karibu miezi miwili.**
>
> Mark Irungu

to yetu kubwa ilikuwa kubuni mfumo utakaobaini anayefaa kupewa pesa hizo. Pili ilikuwa kutafuta jinsi ya kupata pesa zetu kutoka kwa wanaoshindwa kulipa, hata hivyo Mahakama ya Madeni Madogo imetusaidia sana, kwani kesi huchukua miezi miwili.

Changamoto ya tatu ilikuwa kuelewa tabia ya mkopaji. Wakopaji, hata kama ni wa mara kwa mara, huondoka kwa njia tatu: kutafuta mkopo rahisi, kubadilisha maisha na kuishi kulingana na mapato yao ama kukataa kulipa," anaeleza. Kutokana na ufahamu huo, Irungu alibuni mfumo ambao unaweza 'kuwasoma' wateja na kuelewa mtindo wao wa kukopa na kulipa. "Kwa bahati nzuri, huwa tunashughulika na kampuni wala si watu binafsi, hali ambayo hutupa usalama fulani."

Irungu anaendesha biashara nyingine mbili - Ndani Medical Supplies, inayohusika na mashine za matibabu, na Ndani Technologies Africa, inayotoa huduma za teknolojia kwa taasisi za benki, mashirika ya mawasiliano na serikali.

Na huo sio mwisho wake wa kubuni biashara; anasema analenga kuanzisha biashara nyingine tano. "Nikiwa mtoto wa mchungaji, huwa nasoma Biblia sana. Kitabu cha Mhubiri 11:2

kinasema: 'Wekeza katika masuala saba, ndiyo, manane; hujui mkasa ambao huenda ukaikumba nchi.' Kwangu, ni safari ya kuelekea biashara ya nane, na nimechukua masuala yaliyonivutia hapo awali," anasema.

Mfanyabiashara huyo ambaye ni mtoto wa pili katika familia ya watu watatu alizaliwa katika mtaa wa Dagoretti, Nairobi, na wazazi waliozingatia sana Ukristo. Waliishi maisha ya wastani lakini hali iligeuka kuwa ngumu akiwa Kidato cha Pili katika Shule ya Upili ya Highway, jijini Nairobi.

"Nikiwa katika shule ya kutwa ilikuwa vigumu kwani niliona jinsi wazazi wangu walivyoteseka. Kuna wakati nilitumwa nyumbani kwa kutolipiwa karo lakini nikaendelea na shuleni kila siku hadi dawati langu lilipoondolewa darasani na sikuwa na popote pa kwenda," anakumbuka.

Hali ilianza kuimarika akiwa Kidato cha Nne, na baada ya shule ya upili, alijiunga na Chuo Kikuu cha Kimataifa cha Amerika-Africa (USIU) alikosomea Mifumo ya Mitambo na Teknolojia.

Mnamo 2008, alishiriki masomo ya nyanjani katika UNEP na Kituo cha Kilimo cha Misitu Duniani, kabla ya kupata kazi yake ya kwanza rasmi, ambayo alikuwa akilipwa mshahara wa Sh60,000.

Ni kitu gani angependa kubadilisha kuhusu maisha yake ya awali? "Tulipoenda shuleni, kulikuwa na msisitizo mkubwa kuhusu kupita mitihani na kupata alama nzuri. Ningerudi shuleni leo, ningeangazia sana kuhusu uboreshaji wa ujuzi. Ningekuwa wa miaka 19 tena, singepoteza muda kusomea shahada ya Uzamili; ningeangazia sana ukuzaji wa ujuzi."

Funzo moja ambalo amepata katika miaka hiyo yote ambayo amekuwa akifanya biashara ni umuhimu wa "kuamka na kufika." "Lakini kufika kunaweza kuwa na hali ya kutamausha. Unafika katika siku ya kwanza na unafukuzwa; unafika katika siku ya pili, na yule unayetaka kumuona hayupo. Unafika tena na walinzi wanakufukuza. Hata hivyo, uvumilivu ndiyo huleta mafanikio.

Vijana wanapaswa kuwa wavumilivu na hawapaswi kuruhusu mitazamo ya watu wengine kuamua watakachokuwa maishani.

***ambuthia@ke.nationmedia.com***

*- Imetafsiriwa na Wanderi Kamau*




Nation Media Group "Digital Copy"

maoni




■ Wanachotaka Wakuria, Wateso, Wasabaoti na wengine ni kujumuishwa

# Kenya haihitaji kaunti zaidi



KWENDO
OPANGA

Mswada wa Mbunge wa Kuria Mashariki Marwa Maisori Kitaya unaopendekeza kubuniwa kwa kaunti tano mpya za Kuria, Teso, Mlima Elgon, Pokot Mashariki na Mwingi utapata utaungwa mkono na wengi kwa sababu unaafiki dhana potovu kuwa jamii za walio wachache zimetengwa. Kwamba watu wa jamii hizo wamebaguliwa na kunyimwa kilicho chao kihalali na hivyo ziko hatarini.

Watu wa Kitayama wa Wakuria, kwa mfano, wanahisi kuachwa nje na jamii za Waluo na Wakisii katika uliokuwa Mkoa wa Nyanza kabla ya Katiba ya 2010 na sasa wanahisi kuachwa nje na kusukumwa nje na Waluo wanaoishi nao katika Kaunti ya Migori.

Walihisi hivyo wakiwa katika iliyokuwa Wilaya ya Nyanza Kusini, hadi Wilaya yao ya Kuria ilipobuniwa.

Wakati wa kampeni za ugavana katika Kaunti ya Kitui, David Musila, aliyekuwa Mkuu wa Mkoa na mbunge wa zamani, alidai kuwa, kwa sababu magavana wawili kwa kwanza; Julius Malombe na Bi Charity Ngilu walitoka Kitui, ilikuwa haki kwake, anayetoka Mwingi kuwa gavana wa tatu wa kaunti hiyo.

Katika Kaunti ya Nakuru, Gavana Susan Kihika amelaumiwa hasa kupitia mitandao ya kijamii kwa kuteua baraza la mawaziri la watu 10; saba kati yao wakitoka jamii moja. Nafasi zingine tatu zimegawanywa miongoni mwa makabila mengine, kila kabila likipata nafasi moja. Malalamishi dhidi ya Kihika ni kuwa baraza lake la mawaziri halionyeshi sura ya kaunti hiyo iliyo na makabila zaidi ya 40.

Sababu iliyofanya ugatuzi kutajwa kuwa nyota ya Katiba ya 2010, miaka 10 iliyopita ni kuwa ulilenga kugatua mamlaka kutoka katikati, mahali ambapo rasilimali zinagawanywa kwa njia isiyo sawa, hadi ambako watu wanapaswa kuhusishwa maamuzi yanapofanywa kuhusu usimamizi na matumizi ya rasilimali zao.

Ni Sir John Major akiwa Waziri Mkuu wa Uingereza, aliyesema kuwa siasa zinahusu mizozo na mijadala na Bi Theresa May, mmoja wa warithi wake, ambaye alisema siasa sio mchezo kwa sababu maamuzi wanayofanya wanasiasa katika baraza la mawaziri huathiri maisha ya kila siku ya raia. Nchini Uingereza sawa na Kenya, mijadala na mizozo na maamuzi yanayoathiri maisha ya kila siku yanahusu rasilimali na ugavi wake.

Siasa za hasla na mfumo wa kiuchumi wa 'Bottom Up' zinahusu rasilimali ambapo wananchi wa kawaida, wanawake wanaouza mboga na wanaosukuma mikokoteni wanajumuishwa katika siasa na uchumi badala ya mambo haya kutengewa watu wa familia za tangu zamani za kisiasa na kibiashara. Hasa, malalamishi ambayo baadhi ya watu wanatoa dhidi ya serikali yanahusu rasilimali.

Wanachotaka Wakuria, Wateso, Wasabaoti na wengine ni kujumuishwa katika maamuzi kuhusu rasilimali na ujumbe wa Mswada wa Kitayama ni kuwa wachache wametengwa.

Wanachosema Kitayama na wengine katika Bunge la Kitaifa ni kuwa miaka 59 tangu uhuru baadhi ya Wakenya hawahisi kuwa ndani, wanahisi kuachwa nje.

Wanasema Wakenya kama hao wanaweza tu kuhisi kuwa wenyeji na kuwa wanatembea pamoja na wenzao nchini wakipata kaunti zao zitakazobuniwa kutoka kwa wanazoishi sasa. Ni lawama ambayo Kitayama na wenzake wanaelekeza jwa wasimamizi wa kaunti za Migori, Busia, Bungoma na Trans Nzoia, Pokot Magharibi na Kitui.

Makundi ya kikabila hayamaanishi kujumuishwa lakini watu wanaolalamika wanaweza kusamehewa kwa kufikiri wanajumuishwa. Msimamo wangu ni kuwa Kenya haihitaji kaunti zaidi lakini chache, ambapo sheria, maadili na utendaji umewekwa wazi na hakuna eneo au mtu atatengwa kutoka kwa meza ya kufanya maamuzi au kugawa rasilimali.

*kwendo58@gmail.com*

*- Imetafsiriwa na Charles Wasonga*

Nation Media Group "Digital Copy"

maoni

■ KULINDA KATIBA

# Tuondoe dhana hii potovu kuhusu kaunti



MACHARIA
GAITHO

Pendekezo la Mbunge wa Kuria Mashariki Marwa Kitayama la kubuniwa kwa kaunti tano zaidi linaweza kuwa suluhu kwa jamii zinazohisi kudhulumiwa katika kaunti zao wakati huu.

Kuongeza kaunti kutoka 47 hadi 52 kunaonekana kuwa rahisi kama kutashughulikia malalamishi ya makundi yaliyotengwa na makabila makubwa, hata baada ya ugatuzi.

Makabila madogo yamenyimwa nafasi ya kuchagua Magavana, Maseneta, Wabunge Wawakilishi, Maspika wa Mabunge ya Kaunti na viongozi wengine na wawakilishi katika ngazi ya kaunti. Pia wamenyimwa nafasi za ajira na ugavi sawa wa rasilimali.

Haya ni masuala mazito ambayo yanapaswa kushughulikiwa, kwani kuyapuuza huacha kidonda ambacho kinaweza kuleta hisia ya kutengwa na hatimaye kuwa sababu ya uasi.

Hata hivyo, kubuni kaunti mpya pekee hakuwezi kusuluhisha jambo hilo. Hatua hiyo itahujumu kazi yote nzuri iliyofanywa kuunda Katiba ya 2010, na kupeleka Kenya miaka 60 nyuma katika kuunda maeneo madogo ya utawala ya kikabila na kiukoo.

Ikumbukwe kuwa shughuli ya kuunda kaunti iliibua mvutano mkubwa wakati wa majadiliano kuhusu utayarishaji wa katiba. Mwafaka wa kuundwa kwa kaunti 47 ulifikiwa baada ya mvutano kati ya wazo la kuundwa kwa kaunti kwa misingi ya wilaya 200 zilizokuwepo wakati huo au kuongezwa kidogo kwa mikoa minane ya utawala.

Maelezo machache yanafaa. Baada ya kupata Uhuru, Kenya iligawanywa katika wilaya 42 ndani ya mikoa minane. Wakati fulani kati ya miaka ya 1980, Rais Daniel Arap Moi alianza kukuza vigogo wa kisiasa wa kikabila, mkakati uliohusu kuwatengenezea himaya za kikabila ili wazitawale. Alianza kwa kubuni wilaya tano mpya ambazo zilihalilishwa, na kuongeza idadi hadi 47. Zingatia idadi hiyo.

Katika miaka iliyofuata Rais Moi aliendeleza mtindo wa kubuni wilaya kila mahali ambako alihitaji kuwa na kikaragosi fulani wa kisiasa. Ndani ya muda mfupi, idadi ya wilaya iliongezeka maradufu.

Rais Mwai Kibaki alipochukua uongozi 2002, aliahidi kumaliza enzi ya utaoaji maamuzi ya kisera kiholela, lakini baada ya muda mfupi yeye pia aliambukizwa virusi vya wilaya. Maeneo ya utawala yaliyokuwepo yaligawanywa bila udhibiti wowote kiasi kwamba baada ya miaka michache ilikuwa ni kama kwamba kila eneo wanakokaa watu wa kabila fulani liligeuzwa kuwa wilaya.

Ilifikia hatua ya kiajabu wakati ambapo wilaya zilikuwa nyingi kuzidi maeneo bunge, baadhi wabunge wakisimamia maeneo yanayovuka mipaka ya wilaya. Ni hali hiyo ya mtanziko ambayo ilikumba wataalamu walioandika Katiba mpya ilipofika wakati wa kubuniwa kwa kaunti chini ya utawala wa ugatuzi.

Baadhi ya wanasiasa walitaka kila moja ya zaidi ya wilaya 200 igeuzwe kuwa kaunti, jambo ambalo haingewezekana.

Wengine walitaka mikoa minane iliyokuwepo igeuzwe kaunti, lakini mikubwa kama vile Bonde la Ufa na Mashariki igawanywe mara tatu kila moja ili Kenya iwe na kaunti 12.

Mwishowe, mwafaka ulifikiwa ambapo wilaya 47 zilizohalalishwa awali ziligeuzwa maeneo ya serikali ya ugatuzi. Wilaya zingine zaidi ya 150 zilizobuniwa katika enzi za Moi na Kibaki hazikuwa zimehalalishwa kisheria. Misingi na makubaliano yaliyochangia kuundwa kwa kaunti 47 ndiyo Marwa Kitayama, na wanaounga mkono pendekezo lake, wanataka kuvunja. Ni rahisi kuanza na kaunti tano, lakini baadaye huenda kila kabila, ukoo au makundi mengine pia yakataka kuwa na kaunti huru.

Kampeni zaidi za kutaka kuundwa kwa kaunti mpya zitafuta na tusipochunga tutaru kwa kaunti na mabunge 200 au zaidi.

Tayari serikali 47 za kaunti kwa nchi ndogo kama Kenya ni nyingi sana, lakini hayo ni makubaliano yaliyofaa wakati huo.

Kimsingi, nchi ya ukubwa wa Kenya na idadi ya watu haifai kuwa na zaidi ya maeneo 12 ya kiutawala. Hili ndilo suala tunalopaswa kujadili, badala ya majaribio mapya ya kutenga maeneo madogo ya kikabila yasiyo na maana yoyote ila kuridhisha tamaa ya wanaotafuta ukubwa kupitia maeneo hayo madogo.

**Kimsingi, nchi ya ukubwa wa Kenya na idadi ya watu haifai kuwa na zaidi ya maeneo 12 ya kiutawala. Hili ndilo suala tunalopaswa kujadili, badala ya majaribio mapya ya kutenga maeneo madogo ya kikabila yasiyo na maana yoyote ila kuridhisha tamaa ya wanaotafuta ukubwa kupitia maeneo hayo madogo.**

Ni lazima pia tuondoe dhana potovu kuwa maeneo madogo ya utawala na kisiasa yataleta maendeleo "karibu na watu". Kile yanafanya ni kuongeza sehemu zaidi za kiutawala na walafi wa kisiasa ambao sharti wale kutoka nyungu hiyo hiyo na kuwanyima raia rasilimali haba zinazopasa kuwafaidi.

Pendekezo la kubuniwa kwa kaunti mpya sharti lizimwe kabla ya kushika kasi. Hatua ya kwanza ni kwa serikali ya Rais William Ruto na upinzani ukiongozwa na Raila Odinga, kupinga hadharani njama hii ya kubadilisha Katiba. Pia, viongozi hao sharti waagize wabunge na maseneta wa mirengo yao kupinga mswada wowote unaolenga kubuni kaunti mpya.

*** *** ***

Kandanda ya Kombe la Dunia imetujia kwa mara nyingine. Kwa muda wa mwezi mmoja ujao wanaume wote wataelekeza macho na mawazo yao kwa mchuano huo nchini Qatar ukipeperushwa moja kwa moja kupitia televisheni zote.

Inajulikana kuwa kandanda haiwezi kufurahiwa ndani ya nyumba. Kwa hivyo, wanawake wote wanahitajika kutoa "visa za usafiri" kwa wanaume zao kuungana na wengine katika mabaa, vilabu, kumbi za miji na maeneo mengine ya umma ambako mchezo huo utaonyeshwa kutoka Qatar.

Wanapaswa kuhamisishwa kuhusu ukweli kuwa, soka ikiwa mchezo wa dakika 90, kila ziara katika "uga wa michezo" sharti itengewe muda wa saa moja wa maandalizi, na kipenga cha mwisho hufuatiwa na uchanganuzi wa baada ya mechi. Awamu hii inaweza kudumu kutoka saa moja hadi usiku kucha kutegemea utashi na msisimko uliopo.

Manufaa ya wenzetu katika ndoa ni kuwa katika kipindi hicho, watamiliki kifaa cha kubadili stesheni za televisheni ili watazame, bila kuzuiwa au kusumbuliwa, vipindi vyote vya kuigiza vya asili ya Mexico, India, Nigeria na Ufilipino miongoni mwa vingine wanavyopenda.

*gaithomail@gmail.com*

*- Imetafsiriwa na Charles Wasonga*

Nation Media Group "Digital Copy"

BUNGE LA AFRIKA MASHARIKI

# LIMEKUWA JAA LA KISIASA?

**Bunge la kanda linachukuliwa kuwa kituo cha vigogo wa kisiasa wa Kenya kuzawadi washirika au kutupa wanaokataliwa kwenye uchaguzi**




Makao makuu ya Bunge la Jumuiya ya Afrika Mashariki mjini Arusha, Tanzania.

NA OSCAR OBONYO

Alasiri moja mnamo Novemba 2016 ilimpata mbunge wa Kenya akitetea hatua ya kupiga marufuku matumizi ya mifuko ya plastiki katika Bunge la Afrika Mashariki (EALA).

Lakini alikatizwa na mwenzake kutoka Uganda na kuulizwa iwapo alikuwa na habari kuwa asubuhi hiyo Kenya ilikuwa imechapisha ilani ya gazeti rasmi kinyume na kauli yake, jambo lililozua kicheko katika Bunge hilo na mbunge huyo Mkenya kuaibika vibaya.

Ni tukio ambalo liliwapa tope wabunge kutoka Kenya katika bunge hilo lenye makao yake Arusha, anakumbuka aliyekuwa Mbunge wa EALA, Bi Mumbi Ng'aru. "Tulihisi kudhalilishwa na tukachanganyikiwa kama wawakilishi wa nchi. Lakini ili kuondoa aibu, tulichukua hatua ya haraka na kuomba mswada huo usimamishwe kwa muda ili tuwasiliane na maafisa husika nyumbani Nairobi."

Ni wazi kuwa hili lilikuwa suala la mkono wa kushoto kutojua ulichokuwa ukifanya mkono wa kulia. Na ingawa wabunge wa Kenya hatimaye walishauriana na maafisa nyumbani na kufaulu kubadilisha msimamo uliochukuliwa na wadau katika sekta ya plastiki (ambao, chini ya uongozi wa Chama cha Watengenezaji Bidhaa Kenya walikuwa wameshawishi kukataliwa kwa Mswada huo), nchi ilikuwa imejiaibisha kwa kutoratibisha vyema suala hilo.



Aliyekuwa Spila wa EALA Speaker Abdulrahman Kinana.

Tukio hili la 2016 linaonyesha mambo matatu muhimu: uratibishaji duni au kukosekana kabisa kwa ushirikiano kati ya serikali kuu na wabunge wa Afrika Mashariki, serikali kutojali au kutofahamu kabisa shughuli za EALA, na ubora na umakinifu wa wawakilishi wa Kenya katika bunge hilo Arusha. Kwa mfano, ni ajabu kwamba, katika kisa alichotaja Mumbi, mwenzao kutoka Uganda alikuwa akifahamu yaliyokuwa yakiendelea Nairobi kuhusu Mswada husika kuliko mbunge kutoka Kenya.

Mmoja wa wabunge wa kwanza wa EALA, Calist Mwatela, anahusisha nyingi za changamoto hizi na ukweli kuwa serikali za kitaifa zinadaiwa kutokuwa na umakini sana kuhusu EALA na kuwa na haraka ya kuchagua watu wa kuchukua nafasi za wanaoshikilia nyadhifa hizo. Mwatela anasema EALA huwa ni kituo cha vigogo wa kisiasa kuwazawadi washirika wao au wanaokataliwa katika uchaguzi.

Hali kwamba kalenda za EALA na Bunge la Kenya zinawiana huwa rahisi kwa wanasiasa kuchagua washirika wao wanaoshindwa baada ya kampeni kali, na kuwazawadi kwa tikiti ya kwenda jiji la Arusha, Tanzania.

Hata hivyo, huwa hakuna hakika kwa sababu uamuzi kama huo ni lazima uthibitishwe na Bunge la Kitaifa kupitia kwa kura.

Kwa mfano, wabunge tisa walioteuliwa katika EALA iliyopita, watano - ikiwa ni asilimia 56

Nation Media Group "Digital Copy"

- walikuwa watu walioshindwa kwenye uchaguzi mkuu wa 2017 au katika mchujo wa vyama ambao ni Oburu Oginga, Simon Mbugua, Aburi Mpuri, Aden Omar Abdikadir na Muhia Wanjiku.

Hali si tofauti mwaka huu kwa kuwa wengi wa walioteuliwa na vyama tofauti vya kisiasa ni walioshindwa kwenye uchaguzi akiwemo Hassan Omar, aliyegombea kiti cha ugavana Mombasa, Katibu Mkuu wa Jubilee Jeremiah Kioni, aliyeshindwa kuhifadhi kiti chake cha ubunge cha Ndaragwa na wabunge Kizito Mugali (Shinyaju) na Fatuma Gedi (Kaunti ya Wajir).

Uteuzi wa Winnie Odinga na Kennedy Musyoka katika EALA ambao ni watoto wa aliyekuwa Waziri Mkuu Raila Odinga na aliyekuwa Makamu Rais Kalonzo Musyoka mtawalia, umeibua mjadala mkali huku baadhi ya watu, akiwemo mwenyekiti wa chama cha United Democratic Alliance (UDA), Johnston Muthama, akilalamikia kuhusu anachotaja kuwa "viongozi wa kisiasa kutumia vibaya nafasi za ubunge kupeleka watoto na jamaa zao kwa likizo Tanzania".

Madai ya Muthama, yawe ya kweli au uongo, yanaakisi jinsi mwonekano wa EALA ulivyo kwa umma. Kwa wengi, sio mahali pa shughuli muhimu lakini ni kituo cha likizo au kazi rahisi.

Ajabu ni kuwa Kenya sio nchi ya pekee ambayo inateua watoto wa viongozi wakuu katika Bunge hilo. Katika bunge la tatu, kwa mfano, Makongoro Nyerere na Abdullah Mwinyi, ambao ni watoto wa waliokuwa marais wa Tanzania Julius Nyerere na Ali Hassan Mwinyi, waliteuliwa EALA.

Bunge hili lililoanzishwa 2001 na kufanya kikao cha kwanza jijini Arusha Novemba 30, Spika wake wa kwanza akiwa Abdulrahman Kinana wa Tanzania, ni asasi huru ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC). Kwa sasa lina wabunge 62, nchi zote 6 wanachama zikichagua wabunge tisa na maafisa wanane wasio wa kuchaguliwa.

Mwatela, na waliokuwa mawaziri Margaret Kamar na John Koech, ni miongoni mwa wabunge wa kwanza wa EALA. Wengine ni Maxwell Shamala, Ochieng' Mbeo, Rose Waruhiu, Abdilahi Adan, Jared Kangwana na Zubedi Mohamed Abdullah. Wakiwa wa kwanza, wabunge wa Bunge la Kwanza walifanya kazi kubwa ya kuweka kanuni, ikiwemo Muungano wa Forodha, miongoni mwa sheria zingine. Kwa mfano, Mwatela anasema pia walipitisha Rwanda kuwa mwanachama wa nne wa jumuiya hiyo baada ya Kenya, Tanzania na Uganda.

Miradi mingine iliyoshughulikiwa na EALA ni kujengwa kwa vituo vya mipakani vya, jambo ambalo lilishughulikiwa na Bunge la Tatu.

Miji mitatu ya mpakani ya Kenya ya Busia, Lungalunga na Namanga ilikuwa ya kwanza kutambuliwa kwa mradi huo. Lakini pengine shughuli inayokumbukwa ya wabunge wa EALA wa Kenya ni mpango wa uhamasishaji ambapo walitembelea kaunti 37 miongoni mwa 47 kati ya 2013 na 2016, wakielezea raia majukumu na umuhimu wa Bunge hilo na pia mchakato mzima wa ushirikiano.

Licha ya juhudi hizi kubwa, ajenda ya kutunga sheria imekwama kwa miaka - sio kwa kupenda mbali kutokana na makosa ya muundo. Changamoto kubwa ni jinsi miswada inashughulikiwa, tatizo ambalo hulemaza mchakato mzima wa bunge hilo.

Kuna njia mbili za kuwasilisha mswada katika bunge hilo - kupitia mswada wa mwanachama binafsi na kupitia mswada wa baraza la mawaziri wa nchi wanachama. Njia ya kwanza, ambayo hufadhiliwa na mwanachama binafsi huwa na onyo kwamba "utekelezaji wake haufai kuhusisha matumizi ya pesa kutoka kwa nchi wanachama" - kigezo ambacho kinatatiza mchakato wa kutunga sheria.

Mswada unaowasilishwa na baraza la mawaziri una visiki vikubwa zaidi, kulingana na wabunge wa zamani wa EALA, kwa kuwa unahitaji muafaka na ushawishi kutoka kwa wabunge wanaohusika na masuala ya EAC. Nchi wanachama zikifaulu kushawishika, mswada huo hupelekwa kutiwa saini na Wanasheria Wakuu wa kila nchi kabla ya kuwasilishwa kwa viongozi wa nchi, "ambao ni lazima watie saini zao katika kikao kimoja".

Bi Ng'aru anakiri kuwa hii ndiyo njia ndefu na ngumu ya kusukuma miswada kwa kuwa mchakato huo unahitaji ushawishi, ubembelezaji na hata vitisho ili wabunge wote waukubali. Na mswada unaweza kuporomoka iwapo mwanachama mmoja atakataa kutia saini. Ni mchakato ambao wakati mwingine unaweza kuchukua muda mrefu wa hata miaka mitatu.

## Wabunge wa EALA




Mwatela, ambaye baadaye alihudumu kama Mbunge wa Mwatate katika Kaunti ya Taita Taveta kati ya 2007 na 2013, anahusisha hali hii na anachotaja kuwa "kiburi cha uhuru". Huku kila nchi mwanachama ikizingatia na kulinda maslahi yake ya kitaifa kwa kujificha katika uhuru wake, kufanya mambo kwa kusudi moja ni vigumu kuafikiwa.

Mwatela, aliyekuwa waziri msaidizi wa elimu anatoa mfano wa pendekezo lake la kuundwa kwa shirika moja la kusimamia mchakato wa uchaguzi katika nchi zote wanachama, ambalo lilikataliwa kutokana na "sababu za uhuru" kwa kuwa kila nchi ilitaka kuendesha masuala yake.

Mwatela alitaka kuwe na shughuli moja ya uchaguzi katika kanda hatua ambayo lingekomesha madai yasiyoisha ya wizi wa kura. Kukataliwa kwa pendekezo hili kunaibua maswali kuhusu uwezekano wa kukubali mchakato tata zaidi: ule wa kuunda muungano wa kisiasa.

Lakini kwa Mwatela, pengine sababu kubwa ya viongozi wa serikali ya Kenya kutopatia umuhimu Bunge hilo ni ukweli kuwa wabunge waliohudumu katika EALA kwa mihula miwili au hata muhula mmoja katika EALA na mmoja katika Bunge la Kitaifa la Kenya, hawapati pensheni na marupurupu ya kustaafu.

Hii ni kwa sababu inachukuliwa kuwa huwa hawajahudumu kwa mihula mwili mfululizo kama wenzao wa Bunge la Kitaifa na Seneti. Walioathiriwa ni Mwatela na Mbeo, ambaye alihudumu kama mbunge wa Mathare, Nairobi kwa mwaka mmoja kabla ya kujiunga na EALA. Wawili hao waliwasilisha ombi kwa Rais mstaafu Uhuru Kenyatta kuhusu swala hilo, lakini inaripotiwa kuwa hakuchukua hatua.

Huku nchi zingine wanachama zikiteua makamu rais wa zamani, mawaziri wakuu wa zamani na mawaziri wa zamani, Kenya inahitaji kubadilisha mchakato wake wa kuchagua wawakilishi katika EALA. Muthama, anatumai kuwa wakati utafika ambapo Wakenya hawatakumbuka EALA baada ya uchaguzi mkuu lakini watakuwa wakivutiwa na shughuli za bunge hilo katika vikao vyake vyote Arusha.

***oscar.tko@gmail.com***

*- Imetafsiriwa na Benson Matheka*

Nation Media Group "Digital Copy"

SAYANSI NA TEKNOLOJIA

# Google kulipa Sh47 bilioni kuhusu kesi




Kampuni ya Google italipa Sh47 bilioni kuhusu madai ya jinsi imekuwa ikichukua maelezo kutoka kwa watumizi wake. Kampuni hiyo ilibaini maeneo walimo watu walioamua kujitoa kwa huduma yake ya kubaini mtu aliko katika mitambo yao, yalisema majimbo 40 nchini Amerika.

Google imeambiwa inafaa kuwa na uwazi kuhusu kubaini waliko watu katika siku za usoni na kubuni ukurasa maalum mtandaoni unaowaelezea watu kuhusu maelezo inayochukua kutoka kwao. Ndiyo kesi kubwa zaidi inayohusu maelezo binafsi inayojumuisha majimbo kadhaa katika historia ya Amerika.

Akasema afisa wa Google: "Kwa kuzingatia uboreshaji ambao tumekuwa tukifanya katika miaka ya hivi karibuni, tushamaliza uchunguzi huu, uliohusu sera za bidhaa tulizobadilisha miaka mingi iliyopita."

Mwezi uliopita, Google ilikubali kulipa jimbo la Arizona Sh8.5 bilioni kuhusu inavyokusanya maelezo ya waliko watu. Kesi nyingine moja imebaki katika mahakama za Amerika, baada ya Texas, Indiana, Washington na District of Columbia kuchukua hatua za kisheria dhidi ya Google mnamo Januari. Kujua aliko mtu huwasaidia wavumishaji bidhaa kulenga bidhaa za kibiashara. Huduma hiyo pia inaisaidia Google kupata faida ya Sh20 trilioni kila mwaka kutokana na matangazo ya biashara.

Mwanasheria Mkuu wa Oregon, Ellen Rosenblum, aliyeongoza kesi hiyo - na Mwanasheria Mkuu wa Nebraska Dough Peterson - walisema: "Kwa miaka mingi Google imekuwa ikitilia mkazo kupata faida badala ya usalama wa maelezo ya watumiaji wake.

*- Imetafsiriwa na Wanderi Kamau*

# ENZI MPYA KWA SAFARI YA BINADAMU MWEZINI



**Roketi ya Artemis 1 ya kwenda mwezini isiyo na abiria ikitoka katika jukwaa la kuirushia katika kituo cha Nasa cha Kennedy Space Centre eneo la Cape Canaveral, Florida, mnamo Novemba 16. Safari yake itakuwa ya siku 25 na nusu kwenda upande wa mbali wa Mwezi na kurudi.**

LONDON

Kwa mlio wa injini zake zenye nguvu, roketi mpya ya Nasa imetuinua na kuanza enzi mpya ya binadamu kutalii anga.

Nasa wiki hii ilizindua roketi yenye nguvu zaidi kuwahi kutengenezwa kuelekea mwezini katika hafla ya kipekee iliyoashiria mwanzo wa mpango wa utalii wa angani wa shirika hilo, Artemis.

Roketi hiyo yenye urefu wa orofa 32 ilirushwa angani kutoka Kituo cha Anga cha Kennedy, Florida, saa 12.47 alfajiri.

"Mlichofanya leo hii kitavipa msukumo vizazi vingi vitakavyokuja, ahsanteni!" akasema Charlie Blackwell-Thompson, mkurugenzi wa kwanza wa uzinduzi wa roketi wa Nasa, akiwaambia wenzake waliokuwa wakishangilia.

Roketi hiyo imeambatanishwa na roketi ndogo aina ya Orion ambayo haina watu na ambayo itazunguka mwezi, katika jaribio la safari zitakazofanywa katika siku za usoni, ambazo huenda zikamfanya mwanamke wa kwanza na mtu mweusi wa kwanza kutua mwezini kufikia mwaka 2025.

Saa mbili baada ya kuzinduliwa, Nasa ilisema roketi hiyo ilikuwa safarini kuelekea mwezini, na baadaye ikatoa picha za kwanza za Dunia ikipungua katika mwonekano wake kutoka ilikokuwa roketi hiyo angani.

"Sasa tunaelekea tena mwezini, si kufika mwezini tu, bali kufahamu jinsi ya kuishi mwezini ili kujitayarisha kuwatuma wanadamu hadi katika Sayari Mars," msimamizi wa kituo hicho cha Nasa, Bill Nelson, akaambia wanahabari baada ya uzinduzi huo.

"Huu ni mwanzo mpya, hiki ni kizazi cha Artemis," akaongeza Nelson, aliyesema alitazama uzinduzi huo kutoka kwa paa la jengo la kutengenezea roketi akiwa na wanaanga wengine.

Amerika ilituma wanaanga mara ya mwisho mwezini enzi ya Apollo, kutoka 1969 hadi 1972. Wakati huu, inatarajia kufanya zaidi - kikiwemo kituo cha anga mwezini - kusaidia kwa safari yake Mars kufikia miaka ya 2030.

Hali ya hofu ilizuka vikosi vya wataalamu vilipofanya juu chini kurekebisha matatizo ya kimitambo yaliyochelewesha kwa saa mbili uzinduzi huo ulioanza saa 7.04 alfajiri.

Kwanza, wahandisi walilazimika kusimamisha mwelekeo wa gesi ya haidrojeni katika eneo muhimu Jumanne usiku ilipobainika eneo moja lilikuwa likivunja, lakini kundi lililotumwa kukagua uthabiti wa mitambo yake lilisuluhisha tatizo hilo kwa kufunga vizuri komeo zilizokuwa zimelegea.

Baadaye, shirika hilo liligundua mashine ya kufuatilia mwenendo wa roketi hiyo ilikuwa na tatizo la kibonyezo cha mtandao na ikabidi kingine kiwekwe.

Ilikuwa mara ya tatu kwa Nasa, baada ya uzinduzi huo kuahirishwa mara mbili hapo awali kutokana na matatizo ya kimitambo. Uzinduzi huo pia ulichelewa kutokana na matatizo ya hali ya anga kikiwemo Kimbunga Ian, kilichoikumba Florida mwishoni mwa Septemba.

Watu karibu 100,000 walitarajiwa kukusanyika katika ufuo wa pwani ili kushuhudia tukio hilo la kihistoria. Todd Garland aliendesha gari lake kutoka Frankfurt, Kentucky kushuhudia uzinduzi huo kutoka Ufuo wa Coco.

Akiwa amevalia Jezi ya Artemis, Grland, 55, aliambia AFP akibubujikwa na machozi: "Hili limekuwa tukio ambalo nimekuwa nikitamani kushuhudia katika maisha yangu yote.

"Kumbukumbu yangu ya kwanza ni mama yangu akiniamsha nikiwa na umri wa miaka miwili kutazama roketi ikirudi duniani kutoka eneo la mwezi na nimekuwa nikitaka kuona uzinduzi wake kwa muda mrefu, sasa nimeuona."

*- Imetafsiriwa na Wanderi Kamau*

Nation Media Group "Digital Copy"

# kurunzi ya afrika

■ JUHUDI ZA KUTAFUTA AMANI CONGO

# UHURU MSTARI WA MBELE



Aliyekuwa Rais wa Kenya Uhuru Kenyatta akizungumza na wakuu wa kijeshi baada ya kufika mjini Goma, mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, mnamo Novemba 15. Wanajeshi nchini DRC wanakabiliana na wapiganaji wa M23 katika eneo la Kibumba, kilomita 20 kaskazini mwa Goma, maafisa wa usalama walisema.

## Siwezi kupuuza yale ambayo nimeona. Lazima niambie pande zote. Hamuwezi kuendesha mazungumzo wakati kuna janga la kibinadamu, anasema aliyekuwa kiongozi wa Kenya

• KINSHASA

Aliyekuwa Rais wa Kenya Uhuru Kenya alizuru mji mkuu wa mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Goma wiki hii, huku mapigano mapya na waasi wa M23 yakiendelea eneo la kaskazini, na kusababisha maelfu kutoroka.

Wanajeshi katika DRC wanapigana na waasi wa M23 katika eneo la Kibumba, umbali wa kilomita 20 kaskazini mwa Goma, maafisa wa usalama na wakazi walisema.

Siku za hivi majuzi, M23 walitwaa eneo kubwa katika mkoa wa Kivu Kaskazini, na kufanya maelfu ya watu kupoteza makao. Mji wa Kibumba unachukuliwa kuwa kimoja cha vijiji vya mwisho kabla ya Goma, mji wa kibiashara wenye watu milioni moja na ulio karibu na mpaka na Rwanda.

Mnamo Jumanne, uvumi kuwa M23 walikuwa wakikaribia ulifanya watu zaidi kutorokea eneo la Kanyaruchinya, kusini mwa Kibumba, ambako kuna kambi ya watu waliopoteza makao.

Watu karibu 40,000 sasa wako katika kambi hiyo, kulingana na msimamizi wake.

Afisa usalama aliyeomba asitajwe jina, alisema watu walianza kutoroka baada ya kuona wanajeshi wakirudi nyuma kuelekea Goma baada ya kukabiliana na waasi wa M23.

Gavana wa Kijeshi wa Kivu Kaskazini, Jenerali Contant Ndima, alitoa wito kwa watu wadumishe utulivu. "Nataka kuwahakikishia tena. . . . Wanajeshi waaminifu wanadhibiti adui katika milima ya Kibumba," akasema. Mzozo huo umeharibu uhusiano kati ya DRC na nchi jirani ya Rwanda, ambayo serikali yake inalaumiwa kwa kuunga mkono waasi hao.

Kenyatta, akiwa mpatanishi kwa niaba ya mataifa saba wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), aliwasili Goma na kuzuru eneo la Kanyaruchinya. Alisema habari alizosikia "zinavunja moyo". "Siwezi kupuuza yale ambayo nimeona," akasema Kenyatta. "Ni lazima niambie pande zote: Hamuwezi kuendesha mazungumzo wakati kuna janga la kibinadamu."

Bw Kenyatta, aliye katika ziuara ya kikazi nchini humo, alisema alitamaushwa na hali mbaya nchini humo na akalaani vikali mzozo wa kibinadamu unaokumba watu wa Kivu Kaskazini.

"Watoto hawa wote, akina mama na wazee ambao wamekuwa wageni katika nchi yao, bi-

...Endelea Uk 26

Nation Media Group "Digital Copy"

# EAC yazidisha juhudi za amani nchini DRC

Kutoka Uk 25

la kujali tofauti zetu, tuwahurumie. Tuwahurumie kwa kukomesha vita kabla ya kuanza mazungumzo," akasema. "Kile nimeshuhudia ni janga kubwa. Vita hivi lazima vikomeshwa mara moja."

Ziara ya Kenyatta katika DRC ni hatua ya hivi punde ya kidiplomasia ya kuzima mzozo huo unaokumba mashariki mwa nchi hiyo inayozongwa na umasikini.

Rais huyo wa zamani alitua katika jiji kuu la DRC Kinshasa Jumapili kwa mazungumzo, akifuatia ziara ya aliyekuwa rais wa Angola, Joao Lourenco. Jumuiya ya EAC pia imeandaa "mazungumzo ya amani" katika jiji kuu la Kenya, Nairobi mnamo Novemba 21. Jumuiya hiyo pia imekubali kutuma wanajeshi wa kulinda amani mashariki mwa DRC. Wanajeshi wa Kenya waliwasili Goma mwishoni mwa wiki jana, kama sehemu ya operesheni hiyo.

Kenyatta alitoa wito kwa makundi yenye silaha kuziweka chini na kurudi kwa mazungumzo. "Hakuna kinachoweza kupatikana kupitia mtutu wa bunduki," akasema. Waziri wa Mashauri ya Kigeni wa Amerika Antony Blinken alisema alishauriana na mwenzake wa Rwanda Vincent Biruta, wakati wa mkutano wa mataifa 20 yenye uwezo mkubwa duniani (G20) nchini Indonesia.

"Nilisisitiza kuwa Amerika inakerwa zaidi na ghasia zinazoendelea mashariki mwa DRC, na niliitaka Rwanda ichukue hatua kukomesha hali hiyo," akasema kupitia kwa twitter.

Naye Biruta alisema kwa twitter kuwa Rwanda iko tayari kwa mazungumzo ya kuleta amani mashariki mwa DRC na pia kupata suluhu ya kisiasa ya mzozo huo.

Makundi zaidi ya 120 yenye silaha yanazunguka eneo hilo, mengi kutokana na vita vya vya kieneo vilivyoanza mwanzoni mwa karne hii. Kundi la M23, wengi wake wakiwa Watutsi kutoka DRC, lilijitokeza mara ya kwanza 2012 lilipoteka Goma kwa muda kabla ya kufurushwa. Lakini waasi ho walirudi mwishoni mwa 2021 baada ya kutoweka kwa miaka kadhaa, wakidai serikali ya DRC imekataa kutimiza ahadi ya kushirikisha wapiganaji wake katika jeshi la kitaifa, miongoni mwa malalamishi mwengine. Waliteka mji muhimu wa Bunagana kwenye mpaka wa Uganda mnamo Juni. Katika wiki za hivi karibuni, waasi hao wamepta ushindi katika maeneo kadhaa dhidi ya wanajeshi wa DRC na kukaribia Goma. DRC ilifurusha balozi wa Rwanda mwishoni mwa Oktoba baada ya M23 kuanzisha upya mapigano. Ingawa Rwanda imekanusha, ripoti ya Umoja wa Mataifa ambayo haijachapishwa iliyoonekana na AFP Agosti inasema Rwanda ni mshirika wa M23.

Rwanda inalaumu serikali ya DRC kwa kushirikiana na wapigaji Wahutu waliotorokea nchini humo baada ya mauaji ya halaiki ya 1994 nchini Rwanda. Wakati huo huo, aliyekuwa mshauri wa rais wa DRC alishtakiwa Jumatatu kwa madai ya ufisadi katika kesi iliyotokana na video ya kamera iliyofichwa. Vidiye Tshimanga, 46, alifikishwa katika mahakama ya Kinshasa akiandamana na mawakili wanane kujibu mashtaka ya ufisadi, uchochezi na kumkosea kiongozi wa taifa.



Nakariri kuwa Amerika inakerwa na mapigano yanayoendelea mashariki mwa DRC na inatoa wito kwa Rwanda ichukue hatua kukomesha hali hiyo.

Waziri wa Mashauri ya Kigeni wa Amerika Antony Blinken



Wanajeshi wa Kenya na Congo wakilinda uwanja wa ndege mjini Goma, mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, muda mfupi kabla ya aliyekuwa Rais wa Kenya Uhuru Kenyatta kuwasili mnamo Novemba 15.

Mnamo Septemba, Mradi wa Kuripoti Uhalifu na Ufisadi na gazeti la Uswisi la Le Temps zilichapisha ripoti ya uchunguzi kuhusu Tshimanga, ambaye alikuwa mshauri maalumu wa Rais Felix Tshisekedi.

Video hiyo ilimuonyesha Tshimanga akiahidi watu wawili wasiotambuliwa, waliodai kuwakilisha kampuni ya Hong Kong inayoshughulika na madini, kulinda biashara yao nchini DRC. "Tukifanya biashara pamoja, nitachukua sehemu yangu ya biashara hiyo," Tshimang akasema katika video hiyo. Alisisitiza pia uhusiano kati yake na Tshisekedi, akisema alisaidia kufadhili kampeni zake za urais 2018. Video hiyo ilizua malalamisji katika mitandao ya kijamii nchini DRC, ambayo ina utajiri mkubwa wa madini lakini ni maskini na inazongwa na ufisadi.

Ofisi ya rais wa DRC imesema vita dhidi ya ufisadi vimewekwa mbele na serikali ya Tshisekedi. Tshimanga amekanusha mashtaka akisema matamshi yake yalitolewa nje ya muktadha. Mahakama kuamua kesi hiyo ndani ya siku 10.

*- Imetafsiriwa na Charles Wasonga*

Nation Media Group "Digital Copy"



# kurunzi ya dunia

■ LINAKUJA NYUMBANI?

# WAZIMU WA KOMBE TENA

**Kuanzia Ziyech, Neymar na Messi hadi Partey, ulimwengu uko tayari kwa sherehe ya kukata na shoka nchini Qatar ambako wanasoka nyota watakutana ana kwa ana kuwania utukufu wa kimataifa**

• KWENDO OPANGA

Je, fahari wa Afrika watanguruma, nyota kung'aa au tai kupaa zaidi ya robo fainali za mashindano ya Kombe la Dunia la Fifa yanayong'oa nanga leo nchini Qatar? Samuel Eto'o, Rais wa Shirikisho la Kandanda la Cameroon, anatumai timu ya Indomitable Lions itafikia fainali ya mchuano huo mnamo Disemba 18. Na anatabiri kuwa Cameroon itacheza na timu nyingine ya Afrika katika fainali hiyo.

Hakuna timu ya Afrika iliyopita robo fainali, huku Cameroon ikiwa ya kwanza kufika kiwango hicho mnamo 1990, ikifuatwa na Lions of Teranga ya Senegal mnamo 2002 nchini Korea Kusini na Japan mtawalia, na Black Stars ya Ghana mnamo 2010 nchini Afrika Kusini. Black Stars wangefika nusu fainali kama wangeshinda Uruguay iliyotiwa nguvu na Luis Suarez na kuwashinda kupitia mikwaju ya penalti.

Cameroon ndiyo timu iliyofaulu zaidi Afrika ikiwa imeshiriki Kombe la Dunia mara nane. Atlas Lions ya Morocco na Carthage Eagles ya Tunisia zimeshiriki mara sita huku Ghana ikishiriki mara nne nayo Senegal mara tatu.

Eto'o, anasema Kombe la Jules Rimet linakuja Afrika, kwa Cameroon hasa, mnamo Disemba. Paul the Octopus na Shaheen the Camel hawachezi sasa lakini shirika la bima la Lloyd's jijini London na kampuni ya data za spoti OPTA, zina maoni tofauti.

Lloyd's ambao ubashiri wao unajikita kwenye thamani ya bima ya wachezaji na timu inasema kuwa Uingereza, iliyo na bima ya thamani ya dola za Amerika 3.7 bilioni (karibu Sh444 trilioni) ndiyo iliyo na nafasi bora zaidi ya kushinda kombe hilo baada ya kuibuka ya kwanza katika kundi lake na kuchapa Senegal, Ufaransa na Uhispania katika mashindano ya mchujo na Brazil katika fainali. Lloyd's wanajigamba kuwa, kwa kutumia fomula hiyo, ubashiri wao ulitimia kuhusu washindi wa Kombe la Dunia mnamo 2014 na 2018.

OPTA, kwa upande mwingine, wakitumia maarifa kimitambo, wameteua Brazil kuwa timu bora zaidi ya kushinda pambano hilo, lakini pia wanasema kila bao litakalofungwa katika mashindano ya makundi na hasa katika kiwango cha mchujo, litaathiri jinsi timu nyingine zitakavyojiandaa na kupambana kushinda katika mechi zake. OPTA huunga mkono vipaji vya wachezaji huku Lloyd's ikionekana kuegemea mishahara yao.

OPTA inapatia Black Stars ya Ghana uwezekano wa asilimia 0.02 wa kushinda Kombe la Dunia. OPTA inafikiri Ghana ina nafa-

Endelea Uk 28

Nation Media Group "Digital Copy"

kurunzi ya dunia

# Nani walio na nafasi bora ya kushinda Qatar?

Kutoka Uk 27

si bora zaidi ya kushinda kombe hilo kuliko Cameroon, Morocco na Tunisia. Ghana imeorodheshwa na Fifa nambari 11 katika bara la Afrika, Cameroon nambari sita barani na nambari 37 duniani.

Atlas Lions imeorodheshwa ya pili Afrika na 24 duniani. The pride ya Senegal inaongoza Afrika na ni ya 20 duniani.

Baada ya kuibwaga the Pharaohs ya Misri na kunyakua Kombe la Mataifa ya Afrika mwaka jana Lions of Teranga itavutia msisimko mkubwa Qatar. Kwa bahati mbaya, mchezaji nyota Sadio Mane anauguza jeraha.

Lloyd's walishabikia Ujerumani kushinda nchini Brazil 2014 na Ufaransa nchini Urusi 2018, lakini wakati huu hawafanyi hivyo licha ya kuwa Ufaransa ndio mabingwa watetezi wa kombe hilo Qatar na Wajerumani hawawezi kupuuzwa hadi wanapobanduliwa. Lakini historia na hali ya hivi karibuni inaonyesha Ufaransa itakuwa na wakati mgumu Qatar.

Hakuna bingwa mtetezi, isipokuwa tu Brazil mnamo 1962 kuanzia 1958, amewahi kushinda kombe hilo mfululizo. Pili huku Les Bleus ikijivunia mastrika wake hatari Karim Benzema, Kylian Mbappe na Antoine Griezman, hali ya kutokuwepo kwa wachezaji machachari Ngolo Kante na Paul Pogba katikati ya kikosi hicho kunaonekana kuzua uwezekano wa kupunguza makali ya kikosi kilichobakia.

Ujerumani italenga kufikia Brazil kama washindi mara tano wa Kombe la Dunia, lakini kocha mpya Hans Flick, aliyeshinda mara sita na timu ya Bayern Munich, anatamani angekuwa na muda zaidi na kikosi hicho. Alichukua usukani baada ya mtangulizi wake Joachim Low, kushindwa mara mbili, droo moja na kushinda mara moja kabla ya Ujerumani kujiondoa Uefa Euro 2020.

Fifa imeorodhesha Brazil nafasi ya kwanza ikifuatwa na Ubelgiji, Ufaransa, Argentina, Uingereza, Italia, Uhispania, Ureno, Mexico na Uholanzi kukamilisha kitengo cha kumi bora ulimwenguni.


Je, inawezekana kuwa Ubelgiji ndiyo timu isiyotarajiwa na wengi kutamba Qatar ilivyokuwa kwa Croatia mnamo 2018 ambayo iliwaacha wengi vinywa wazi kwa kufika katika fainali? Aliyekuwa nahodha wa timu ya Uingereza, David Beckham, anaonelea kuwa wachezaji katika mchuano huu wa Kombe la Dunia wamecheza mechi chache za timu za vilabu na kitaifa, hali inayowafanya kuwa katika hali bora, wenye nguvu na motisha zaidi.

Nani atakuwa nyota wa Kombe la Dunia Qatar? Lionel Messi angependa sana kukunja jamvi kwa kunyanyua kombe hili ambalo limemkwepa kwa muda mrefu.

Neymar Junior analiwinda kwa Brazil, Harry Kane na mchezaji mwenza Son Heung-min wanalisaka kwa Uingereza na Korea Kusini mtawalia, kisha kuna tuzo la Golden Boot kwa mfungaji mabao nyota katika mchuano huo.

Jambo moja ni hakika; kwa siku 29 zijazo, ulimwengu utaelekeza macho Qatar huku mashabiki wa mchezo mashuhuri zaidi wa spoti duniani wakifuatilia timu zao kupitia mechi za makundi, mchujo na hatimaye fainali itakayochezwa Disemba 18.

*- Imetafsiriwa na Mary Wangari*




Nation Media Group "Digital Copy"

kurunzi ya dunia

MADAI YA UFISADI, KURA KUBADILISHWA, NA MIPANGO YA BIASHARA

# KIVUMBI CHA KASHFA

## Qatar imezua fadhaa na hasira katika miaka 12 tangu Fifa iliposhangaza dunia kwa kuipatia haki ya kuwa mwenyeji wa shindano kubwa la soka

• LONDON

'Sasa Mambo Yote' ndiyo kauli mbiu rasmi ya Kombe la Dunia Qatar. Ujumbe ambao, pengine, unalenga hali ya sasa - na mchuano unaokaribia uwanjani.

Tusahau yaliyopita. Laiti ingekuwa rahisi. Ni ajabu kuwa Qatar 2022 inachukuliwa na wengi kuwa tukio kubwa la michezo lenye ubishi mkali zaidi kuwahi kutokea kwa miaka mingi.

Na baada ya yote, ushindani wa hafla kama hii huwa mkubwa. Katika miaka 20 iliyopita, China imekuwa mwenyeji wa mashindano ya Olimpiki mara mbili. Katika muongo mmoja uliopita, Urusi imeandaa Michezo ya Msimu wa Baridi na Kombe la Dunia la Soka 2018.

Na licha ya kiwango cha ukiukaji wa haki za binadamu unaofanya nchi hizo mbili kulaumiwa - na hofu kuwa hafla kama hizo zimetumiwa kutia nguvu tawala za kiimla - ni Qatar inayoweza kusemekana kuzua fadhaa na hasira katika miaka 12 tangu Shirikisho la Soka Ulimwenguni Fifa liliposhangaza ulimwengu kwa kuipatia haki za kuwa mwenyeji wa shindano kubwa la soka.

Ahadi iliyopo ni kuwa Kombe la Dunia la kwanza Mashariki ya Kati litakuwa shindano la kuvutia ambalo linapaswa kusherehekewa.

Hafla ambayo kila mmoja atakaribishwa, kukuza mchezo huo, kuhamasisha vijana, kupiga jeki utalii, kupanua uchumi wa nchi hiyo na kuinua uendelevu. Na huku taharuki katika eneo hili ikilegezwa baada ya majirani wa Qatar kuondoa vikwazo vya kiuchumi dhidi yake mwaka jana, kuna matumaini kwamba hafla hii inaweza kuwa ya kuunganisha.

Lakini hakuna pingamizi kwamba maandalizi ya shindano hili hasa yamekuwa na tatizo.

### Kura na mafarakano

Punde tu rais wa Fifa aliyeondolewa ofisini Sepp Blatter alipotangaza ushindi wa Qatar kuandaa Kombe la Dunia 2010, ilitiliwa shaka jinsi nchi hii ndogo ya jangwa - ambayo haina historia katika Kombe la Dunia na yenye joto kali - ilishinda haki hizo.


Madai ya ufisadi, kura kubadilishwa, na mipango ya biashara katika viwango vya juu vya serikali ni madai ambayo yamekuwa yakikanushwa na waandalizi na hayajawahi kuthibitishwa.

Lakini haiwezi kupuuzwa kuwa wanachama 22 wa kamati kuu ya Fifa ambao walipiga kura siku hiyo miaka 12 iliyopita, na maafisa wengine ambao tayari walikuwa wamesimamishwa, gazeti lilipofichua walikuwa wameitisha pesa ili kuuza kura za Kombe la Dunia, wengi wamelaumiliwa, kupigwa marufuku au kuhusishwa na madai ya ufisadi na kutenda makosa. Hivi majuzi 2020 - kama sehemu ya uchunguzi mpana wa FBI kuhusiana na shirikisho simamizi la soka - waendesha mashtaka wa Amerika walilaumu maafisa wakuu wa Fifa kwa kupokea hongo kwa kupigia kura Qatar.

### Vifo vya wafanyakazi wahamiaji na hofu ya LGBT

Kilichoharibu zaidi sifa za hafla hiyo ni hofu kuhusu vifo vya watu katika ujenzi wa miundomsingi inayohitajika, katika muda mfupi na katika hali kali ya anga, na sheria za kibaguzi zinazoharamisha mapenzi wa watu wa jinsia moja, na kukadamiza uhuru wa wanawake kupitia sheria za kuwataka wasimamiwe na wanaume.

Maafisa wa serikali wanasema kumekuwa na vifo vitatu 'vinavyohusishwa na kazi' katika maeneo ya ujenzi wa viwanja tangu kazi ilipoanza 2014 - na vifo 37 nje ya maeneo ya ujenzi ambavyo "havina uhusiano na kazi".



Aliyekuwa Rais wa Fifa Sepp Blatter

Kamati Kuu inaapa kuwa maslahi ya wafanyakazi ni muhimu. Takwimu rasmi zinaonyesha kuwa raia wasio wa Qatar 15,000 walikufa nchini humo kati ya 2010 na 2019.

Maafisa wa serikali wanasisitiza kuwa idadi hiyo inalingana na ya wafanyakazi wa nchi za kigeni katika nchi hiyo. Lakini idadi ya vifo vinavyohusishwa na kazi - na iwapo kazi hiyo ilihusishwa na Kombe la Dunia - imezua ubishi na haijabainika. Hata bila takwimu rasmi au mageuzi ya leba ya hivi majuzi, wanaoendesha kampeni wanasisitiza kuwa shindano hili litabakia kupakwa damu.

### Kombe la Dunia linaweza kuleta mageuzi ya kijamii?

Qatar 2022 bila shaka imelazimisha spoti kuwaza ni kiwango gani mashindano kama hayo yanaweza kuleta kuhusu mabadiliko ya kijamii. Ni vigumu kusema kuwa kuandaa hafla kubwa za michezo Urusi na China, kwa mfano, kuliongeza kasi ya mageuzi.

Wengi wanakubali kuwa mageuzi ya kikazi Qatar hivi majuzi - ya kuleta ulinzi zaidi kwa wafanyakazi, kuwekwa kwa kiwango cha chini zaidi cha mshahara na kubomoa mfumo wa ufadhili wa 'kafala' - yametendeka kwa sababu ya kupigwa darubini na jamii ya kimataifa ambako kumetokana na Kombe la Dunia.

Hata hivyo, makundi ya kutetea haki za binadamu pia yanasema mageuzi hayo hayajatekelezwa kikamilifu. Na wanashangazwa na kushindwa kwa serikali kufungua Kituo cha Wafanyakazi Wahamiaji, na hazina ya fidia kwa familia za wanaouawa au kujeruhiwa.

### 'Kuzingatia soka'

Ni dalili ya hisia zinazohusiana na hafla hii, na migawanyiko iliyozua, kuwa baadhi ya majina makubwa katika mchezo huu yamejipata yakivutwa kwenye mijadala hii.

Aliyekuwa mlinzi wa Uingereza Gary Neville, kwa mfano, amelaumiwa kwa kukubali kuwa mchanganuzi wa mechi za Kombe la Dunia katika TV inayomilikiwa na Qatar, huku rafiki yake wa karibu David Beckham akikosolewa pia kwa sababu sawa - akiwemo Eric Cantona, aliyekuwa mchezaji maarufu wa Manchester United – kwa kukubali kazi ya kuwa balozi wa hafla hiyo.

Wakati huo huo, Fifa ilizua hasira kwa kuhimiza timu zinazoshindana "kuzingatia soka" kuliko "kuvutwa katika kila shindano la kinadharia na au kisiasa".

*- Imetafsiriwa na Benson Matheka*

Nation Media Group "Digital Copy"

TANZIA

■ TUZO YA EMMY KWA UFANISI MAISHANI

# HUZUNI 'SIKU ZA MAISHA YETU'

## Aniston, mwigizaji mzaliwa wa Ugiriki aliyeigiza kama Victor Kiriakis katika vipindi zaidi ya 3,000 vya Televisheni Amerika kwa zaidi ya miongo mitatu, aaga dunia akiwa na miaka 89

• NEW YORK

John Aniston, nyota aliyeshinda tuzo ya Emmy ya sinema iliyovuma "Days of Our Lives" na baba ya Jennifer Aniston, aliaga dunia wiki hii akiwa na umri wa miaka 89.

Bintiye alimuomboleza Jumatatu asubuhi kwenye Instagram, akitangaza kuwa alifariki dunia Ijumaa, Sikukuu ya Wanajeshi Waliostaafu. John alihudumu katika Jeshi la Majini Amerika.

"Baba mpendwa… John Anthony Aniston," Jennifer Aniston akaandika. "Ulikuwa mmoja kati ya binadamu wa kupendeza zaidi niliowahi kufahamu. Nimejawa na shukrani kuwa ulipaa mbinguni kwa amani - na bila uchungu. Na zaidi tarehe 11/11! Daima ulikuwa stadi wa kuwahi saa. Nambari hiyo sasa itakuwa na maana hata zaidi kwangu milele."

John alitamba kupitia uigizaji katika "Search for Tomorrow", "The West Wing" na "Gilmore Girls". Lakini alipata umaarufu zaidi kupitia mhusika aliyeigiza kwa muda mrefu zaidi katika "Days of Our Lives".

Mnamo 2017, kazi yake katika "Days of Our Lives" ilimwezesha kuteuliwa kwa tuzo ya Emmy kwa mwigizaji bora katika vipindi. Uigizaji huo ulimpa tuzo mbili za Soap Opera Digest - kwa nafasi ya mwigizaji mkuu na mwigizaji mwovu nyota - mnamo 1986, na kuteuliwa kuwa mwigizaji mshiriki katika tuzo la Daytime Emmys mnamo 2017.

Mapema mwaka huu, alikabidhiwa tuzo ya maisha ya Emmy, ambapo Jennifer Aniston alirekodi video kwa heshima yake. "Kando na kuwa fursa hii ni ya kumuenzi shujaa wa kweli katika televisheni ulimwenguni, ni fursa pia ya kutambua ufanisi wake maishani wa kuwa mwigizaji stadi na aliyeheshimika kote, ambaye ni baba yangu," akasema Jennifer Aniston wakati huo.


"John Aniston amekuwa akifanya kazi katika televisheni mfululizo kwa zaidi ya nusu karne. Kwa zaidi ya miaka 30, kujitolea kwake kwa dhati katika kipindi hicho kumemletea heshima na kuwavutia waigizaji wenzake, marafiki wa dhati na kusisimua mamilioni ya mashabiki kote duniani," akasema.

John ameigiza katika vipindi zaidi ya 3,000 vya sinema ya "Days of Our Lives". Taarifa iliyotumiwa TV Line na produsa mkurugenzi wa Days, Ken Corday, ilisema: "ni kwa moyo mzito kwamba tunathibitisha kifo cha mmoja wetu - mwigizaji wetu mpendwa na maarufu, rafiki wa dhati John Aniston. Kwa hakika ni vigumu kutafakari kuwa hatasimama jukwaani tena, lakini ni faraja kwetu sote kufahamu kuwa amepumzika na hahisi uchungu tena."

Kuhusu sifa ya mwigizaji huyo, Corday aliongeza: "Yeye, pamoja na Victor Kiriakis wetu, watasalia nyoyoni zetu milele. Tunatumia familia yake na wote waliomjua upendo wetu na faraja."



Mwigizaji Jennifer Aniston na baba yake, mwigizaji John Aniston, wakihudhuria sherehe Hollywood, Februari 22, 2012.



Mwigizaji John Aniston akihudhuria hafla ya 29 ya kila mwaka ya tuzo za People's Choice Pasadena, California, Januari 12, 2003.

Aniston alioa mara mbili. Alimuoa mwigizaji Nancy Dow, ambaye ni mama yake Jennifer, kutoka1965 hadi 1980. Kisha alimuoa Sherry Rooney 1984. Alikuwa na watoto wawili, Jennifer na Alexander Aniston, na mwana wa kambo John Melick.

Justin Theroux, Kaley Cuoco na Naomi Watts ni miongoni mwa watu mashuhuri walioonyesha upendo wao wakijibu ujumbe wa Jennifer Aniston.

"Natuma upendo mwingi," Watts akaandika. Mapema mwaka huu, John alipokea Tuzo ya Maisha ya Daytime Emmy. Ingawa hakujitokeza katika hafla hiyo, Jennifer alipokea tuzo hiyo kupitia mtandao kwa niaba yake.

John alizaliwa katika Kisiwa cha Crete, Greece, Julai 24, 1933. Alihamia Amerika na familia yake akiwa na umri wa miaka miwili. Familia hiyo ilipata makao jijini Chester, Pennsylvania, ambako John alifuzu kutoka Chuo Kikuu cha Pennsylvania kwa shahada ya digrii katika Sanaa ya Maigizo.

Alianza taaluma yake ya uigizaji mnamo 1962 kama mhusika mdogo katika filamu ya '87th Precinct'. Kuanzia 1970, John alianza kuonekana mara kwa mara katika vipindi vya televisheni, akijitokeza kwa mara ya kwanza katika 'Days of Our Lives' kama mhusika kwa jina Eric Richards.

Kisha aliigiza kama mhusika mkuu katika sinema ya Love of Life kwa jina Eddie Aleata, Search for Tomorrow kama Martin Tourneur, na hatimaye Days of Our Lives mnamo 1985 kama Victor Kiriakis, mhusika aliyeigiza hadi 2021. Risala za rambirambi zimekuwa zikimiminika kwa mwigizaji huyo aliyependwa sana.

*- Imetafsiriwa na Mary Wangari*

Nation Media Group "Digital Copy"

# GET YOUR FAVOURITE DAILIES DELIVERED TO YOUR HOME

Fresh and unbiased news delivered to your doorstep





**SMS the word GAZETI to 20567,**
Share your preferred delivery location
and our agent will get in touch with you

**FREE SMS text and FREE Delivery**

DAILY NATION | Business Daily | TAIFA LEO | The EastAfrican

Terms & Conditions apply*


SPORT ON!
JAMES
WOKABI
BERNARD
NDONG
HOSTS
NATIONFM 96.3 FM
WHERE GOOD MUSIC LIVES
SATURDAYS 3PM